This is a digital copy of a book that was preserved for generations on library shelves before it was carefully scanned by Google as part of a project to make the world's books discoverable online.

It has survived long enough for the copyright to expire and the book to enter the public domain. A public domain book is one that was never subject to copyright or whose legal copyright term has expired. Whether a book is in the public domain may vary country to country. Public domain books are our gateways to the past, representing a wealth of history, culture and knowledge that's often difficult to discover.

Marks, notations and other marginalia present in the original volume will appear in this file - a reminder of this book's long journey from the publisher to a library and finally to you.

Usage guidelines

Google is proud to partner with libraries to digitize public domain materials and make them widely accessible. Public domain books belong to the public and we are merely their custodians. Nevertheless, this work is expensive, so in order to keep providing this resource, we have taken steps to prevent abuse by commercial parties, including placing technical restrictions on automated querying.

We also ask that you:

+ *Make non-commercial use of the files* We designed Google Book Search for use by individuals, and we request that you use these files for personal, non-commercial purposes.

+ *Refrain from automated querying* Do not send automated queries of any sort to Google's system: If you are conducting research on machine translation, optical character recognition or other areas where access to a large amount of text is helpful, please contact us. We encourage the use of public domain materials for these purposes and may be able to help.

+ *Maintain attribution* The Google "watermark" you see on each file is essential for informing people about this project and helping them find additional materials through Google Book Search. Please do not remove it.

+ *Keep it legal* Whatever your use, remember that you are responsible for ensuring that what you are doing is legal. Do not assume that just because we believe a book is in the public domain for users in the United States, that the work is also in the public domain for users in other countries. Whether a book is still in copyright varies from country to country, and we can't offer guidance on whether any specific use of any specific book is allowed. Please do not assume that a book's appearance in Google Book Search means it can be used in any manner anywhere in the world. Copyright infringement liability can be quite severe.

About Google Book Search

Google's mission is to organize the world's information and to make it universally accessible and useful. Google Book Search helps readers discover the world's books while helping authors and publishers reach new audiences. You can search through the full text of this book on the web at `http://books.google.com/`

600094661W

MASOMO

YA

AGANO JIPYA.

SO
LI
DEO
GL
OR
IA

ZANZIBAR, 1881.

101. i. 601

FAHIRISI.

I.	Uzazi wa Yohanna Mbatizaji . . .	1
II.	Uzazi wa Bwana wetu Isa Masiya . .	3
III.	Wachunga waja, Isa atahiriwa, akipewa jina	5
IV.	Isa aletwa hekaluni	8
V.	Kuja Wamajusi, kukimbia hatta Misri, kuuawa wasio na hatiya . . .	10
VI.	Utoto wa Isa, Isa pamoja na Waalimu katika hekalu	13
VII.	Kuhubiri Yohanna Mbatizaji . . .	15
VIII.	Watu waliokuja kwa Yohanna Mbatizaji	17
IX.	Wajumbe wapelekwa kwa Mbatizaji kuuliza, Nani wee?	20
X.	Ubatizo wa Bwana wetu	22
XI.	Jaribu la Bwana wetu Isa . . .	23
XII.	Wafuasi wa kwanza wa Isa . . .	25
XIII.	Kufungwa na kuuawa Yohanna Mbatizaji	27
XIV.	Arusi kwa Kana ya Galilaya . . .	28
XV.	Isa kwa Nazareti	30
XVI.	Mafundisho ya Bwana wetu . . .	31
XVII.	Mitume thenashara	34
XVIII.	Mwanamke wa Samaria	37
XIX.	Masiya awabariki watoto . . .	40
XX.	Miujiza ya Bwana wetu Isa Masiya .	41

XXI.	Isa atuliza bahari na kutembea juu yake.	44
XXII.	Isa alisha watu nyikani	45
XXIII.	Bwana wetu awaponya walioombewa kwake, naye asamehe thambi . . .	48
XXIV.	Bwana wetu Isa Masiya awafufua wafu.	51
XXV.	Mifano ya Bwana wetu	55
XXVI.	Utukufu wa Bwana wetu. . . .	61
XXVII.	Siku za mwisho za duniani za Bwana wetu	63
	Siku ya Juma a pili	64
	Juma a tatu hatta juma a tanu . .	66
	Siku za Alhamisi na Juma . . .	70
	Siku ya Juma a pili	78
XXVIII.	Kupaa Bwana wetu mbinguni . . .	80

MASOMO YA AGANO JIPYA.

SOMO LA KWANZA.

Uzazi wa Yohanna Mbatizaji.

(Luk. I. 1—25, 57—80.)

Palikuwa katika Yerusalemi, karibu na wakati wa kuzaliwa Bwana wetu Isa Masiya, mkohani aliyeitwa Zakariya, na jina la mkewe Elizabeti. Wakaenda wote katika amri za Bwana wakampendeza Muungu, lakini hawana mtoto.

Katika kazi za mkohani zamani zile kuvukiza uvumba katika hekalu jioni, watu wakisimama 'nje wakimwomba Muungu. Ndiyo zamu yake Zakariya aitende hiyo. Akaingia hekaluni avukize uvumba.

Hatta akivukiza, malaika wa Bwana akamtokea upande wa mathbahu ya uvumba, naye Zakariya akimwona malaika, akaingiwa na hofu.

Malaika akamwambia, Usiogope, kuomba kwako kumesikiwa, naye mkeo Elizabeti atakuzalia mwana, utamwita jina lake Yohanna. Utaona furaha na kucheka, wengi watafurahiwa akizaliwa. Malaika akamwambia ginsi atakavyoishi Yohanna, naye atakavyotenda, na

kama atamtangulia Bwana, awaonye watu wamkaribishe. Ndiyo ya kwamba Yohanna atakuwa mhubiri mkuu, atakayewaambia watu ya kuwa Bwana Isa Masiya anawajia.

Zakariya ameomba marra nyingi apewe mwana, illa sasa malaika alipomwambia ya kuwa kuomba kwake kumesikiwa, akaanza kuona shaka, kwa sababu na yeye na mkewe wazee, akanena, Kwa ishara gani nijue ya kwamba haya yatakuwa?

Malaika akamwambia, Ndimi Jibrili, nimepelekwa niseme nawe, nikuonyeshe habari hizi za furaha, nawe utakuwa bubu wala hutaweza kunena hatta haya yatakapokuwa, kwa sababu hukusikia maneno yangu, yatakayotimia wakati wao.

Watu wamekuwa wakingoja, wakataajabu Zakariya akikawia hivi katika hekalu, hatta alipotoka hawezi kusema nao, wakajua ya kwamba ameona njozi.

Wakati wake Elizabeti ukawadia azae, akamzaa mwana. Majirani na jamaa zake wakasikia ya kwamba Bwana amemfanyia rehema kuu, wakafurahi pamoja naye.

Hatta siku ya nane wakaja wamtahiri mtoto kwani killa mtoto mume Myahudi angalitahiri-

wa kwa amri ya Muungu aliyopewa Ibrahimu. Mtoto akapewa jina wakati wa kutahiriwa, kama Wamasihiya wanavyowapa watoto wao majina katika ubatizo.

Wale waliokuwako na Elizabeti na mwanawe wakasema, aitwe Zakariya kama babaye. Illa Elizabeti aliyejua alivyoambiwa baba wake na malaika, akanena, Sivyo, ataitwa Yohanna. Marafiki yake wakamwambia, Hapana katika jamaa zako mwenyi jina hilo. Wakampungia baba wake kujua apendavyo kumwita. Akataka cha kuandikia, akaandika, Jina lake Yohanna. Wakataajabika wote. Marra ulimi wake Zakariya ukalegea, akanena, akamsifu Muungu.

Mtoto akakua akapata nguvu rohoni il a akakaa miaka mingi nyikani, wala watu hawakusikia neno hatta wakati ulipofika, Muungu alipomwita, atoke awahubirie watu wa Israeli.

SOMO II.

Uzazi wa Bwana wetu Isa Masiya.

(Matt I. Luk. I. 26—38. II. 1—7.)

Miezi sita baada ya kumtokea Zakariya Jibril, malaika yule alipelekwa na Muungu kwa mji wa Galilaya ulioitwa Nazareti, kwa mwana mwali aliyeitwa Maryamu. Maryamu hajaole-

MASOMO

YA

AGANO JIPYA.

SO
LI
DEO
GL
OR
IA

ZANZIBAR, 1881.

101. i. 601

mu wachunga kondoo, waliokaa usiku wakiwalinda makundi yao. Akawatokea Malaika wa Muungu, na utukufu wa Muungu ukawang'aria wakaingiwa na hofu nyingi.

Malaika wa Muungu akawaambia, Msiogope, kwani nawaletea habari njema za furaha kuu, zilizo kwa watu wote. Kwani kwa ajili yenu leo, katika mji wa Daud amezaliwa Mwokozi, ndiye Masiya Bwana. Na ishara kwenu ndiyo, Mtamwona kitoto akifungwa na nguo za kitoto, akilazwa malishoni. Marra walikuwako na Malaika wengi wa jeshi la mbinguni wakimsifu Muungu, wakinena, Utukufu kwa Muungu juu, na chini amani, nia njema kwa watu.

Hatta Malaika walipokwenda zao wachunga wakaambiana, Twende sasa hatta Betlehemu, tuone jambo, Muungu alilotujulisha. Wakaja hima, wakaona Maryamu na Yusuf na Mtoto akilala malishoni. Walipokwisha kuona wakatangaza maneno waliyoambiwa ya mtoto huyo. Wote waliosikia wakataajabu kwa mambo waliyoambiwa na wachunga. Illa Maryamu akayashika haya yote, akayafikiri moyoni. Wachunga wakarudi, wakimtukuza na wakimsifu Muungu kwa mambo yote waliyoyasikia wakayaona, kama walivyoambiwa.

Wachunga hawa wangalijua ahadi za Muungu, kwani Malaika asema nao kama walivyo na habari za Masiya Bwana. Maana ya Masiya ndiyo aliyetiwa mafuta. Kama Daudi katika zaburi ametangulia kumnena Mwana wa Muungu aliyetiwa mafuta. Katika zaburi ya pili twasoma, Wafalme wa dunia waondoka, na wakuu wamefanya shauri pamoja, juu ya Yahuwa, na juu ya Masiya yake. Na katika sura ya nne ya Matendo ya Mitume, waanafunzi wakiomba pamoja, wakikumbuka zaburi ile, wakinena, Wafalme wa dunia wameondoka, na wakuu wamekusanyika juu ya Bwana, na juu ya Masiya yake. Daniele tena alitoa unabii wa Masiya mfalme. (Dan. IX. 25.)

Wachunga na Wayahudi wote waliomcha Muungu, na waliofikiri Maandiko Matakatifu, wakamtazamia Mwokozi atakayekuja aliyenenwa nayo Maandiko. Hivi halafu Isa mwenyewe aliposema na Andrea, Andrea akamtafuta ndugu yake Siman, akamwambia, Tumemwona Masiya. (Yoh. I. 41.)

Wakati ule Filipo wa Betsaida akamkuta Natanael, akamwambia, Tumemwona aliyeandikiwa na Musa katika torati, na manabii, ndiye Isa wa Nazareti.

Tumeona ya kwamba kwa sheria ya Musa killa mtoto mume katika Wayahudi akatahiriwa. Hatta Bwana wetu, akiwa Mwana wa Muungu, akaitii sheria, akatahiriwa kama watoto Wayahudi wangineo siku ya nane, akapewa jina, akaitwa Isa, ndilo jina alilolinena Malaika mbele hajazaliwa. Maana ya Isa ndiyo Mwokozi wa Muungu. Malaika aliyesema na Yusuf katika ndoto, ndiye aliyemwambia amwite mtoto kwa jina hili, akamwonyesha maana yake.

SOMO IV.

Isa aletwa Hekaluni.

(Luk. II. 22—39.)

Kwa sheria ya Musa imempasa killa mwanamke aliyezaa mtoto mume wa kwanza, aonekane mbele ya Muungu siku ya arobaini, alete na sadaka. Akiwa na mali alete mwana kondoo wa mwaka wa kwanza, na njiwa ao hua, illakini akiwa masikini alete hua wawili ao njiwa wawili walio wachanga.

Bassi wakati walioamriwa, Maryamu na Yusuf wakamleta mtoto mtakatifu Isa, wamtoe mbele ya Muungu. Na kwa sababu ya kuwa Maryamu maskini hakupata kuleta mwana

kondoo, akaleta kwa amri ya sheria njiwa wawili. Hivi akaletwa Isa hekaluni mwa Yerusalemi.

Bassi palikuwako katika Yerusalemi mtu, jina lake Simeon, aliye wa haki na mcha Muungu, akimngoja yule atakayekuwa faraja ya Israeli, aliyemsomea katika manabii, akamtazamia Masiya. Roho Mtakatifu alikuwa kwa mtu huyu mwema, amemwonyesha ya kwamba hataona kufa asipokuwa amemwona aliyeahidika, Masiya wa Muungu.

Bassi Simeon mwema akaletwa hekaluni na Roho Mtakatifu hatta wazee wake walipomleta mtoto Isa, wamfanyie kwa dasturi ya sheria, akamtwaa mikononi mwake, akambariki Muungu akisema, Umeniruhusu sasa, Bwana, mtumwa wako, kama ulivyosema, niende zangu kwa amani. Kwani macho yangu yameuona wokovu wako, ulioufanya usoni pa watu wote; nuru ya kuwaonya mataifa na utukufu wa watu wako Israeli.

Wimbo huu ndio tuuimbao killa jioni, kumshukuru Muungu aliyetuonya Mwana wake, ndiye Isa Masiya, wokovu ao mwokozi wa watu wote. Ndiye heshima yao Wayahudi, illakini atoa nuru kwa sisi na kwa watu wote, hatta

tukifa, tukimjua yeye, twaweza kwenda zetu kwa amani.

Mtu wa pili aliye mtakatifu akaja kumwamkia mtoto Mwokozi. Ndiye Anna mwanamke mzee sana, mwenyi miaka themanini na minne, aliyefiwa zamani na mumewe, aliyekaa sana hekaluni; akimtumikia Muungu kwa kuomba na kufunga. Akiingia wakati ule na yeye akafurahiwa sana, akamshukuru Muungu, akawapasha habari wote waliotazamia wokovu katika Israeli.

Bassi walipokwisha kutimiza yote yaliyowapasa kwa sheria, Maryamu na Yusuf wakarudi na mtoto hatta Betlehemu. Hawakurudi Nazareti illa baada ya safari iliyo kuu.

SOMO V.

Kuja Wamajusi, Kukimbia hatta Misri, Kuuawa wasio na hatiya.

(Matt. II. 1—18)

Alipozaliwa Isa, Herode mkuu ndiye aliye mfalme wa Wayahudi. Alikuwa chini ya uwezo wa Kaisari ya Rumi, kama tulivyoona, illakini alikuwa mfalme mkuu, akapenda sana ufalme wake. Ameliongeza sana hekalu, akajenga majengo mazuri sana. Lakini Herode alikuwa

mwivu sana, akaua watu wengi pasipo rehema.

Hatta alipozaliwa Isa wakaja Wamajusi wa Mashariki hatta Yerusalemi, wakiuliza, Yuko wapi aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Kwani tumeona nyota yake katika Mashariki, naswi tumekuja tumsujudie.

Hatujui ginsi walivyofundishwa na Muungu ya kwamba nyota waliyoiona ndiyo ishara ya kuzaliwa Mfalme, lakini wakiitambua marra wakaacha nyumba zao, wakaja safari kuu kumfanyia heshima. Walithani labuda ya kwamba mfalme hana buddi kuzaliwa katika mji mkuu, wakaja Yerusalemi, wala hawakuona tena nyota. Herode akisikia akaogopa kama ufalme wake utapotea akija mfalme mwingine, wala hakutaka kumwona Masiya. Akakusanya waalimu akawauliza, Masiya azaliwe wapi? Wakamwambia, Katika Betlehemu, kwani ndivyo walivyosema manabii. Hawa waalimu walikwitwa Waandishi kwa sababu ndiyo kazi yao kuandika na kusahihisha vitabu vitakatifu. Hivi wakapata kujua sana maneno yote ya msahafu.

Herode akisikia majibu yao akawaita Wamajusi akawapeleka hatta Betlehemu, akawauliza wakati ilipokwanza kuonekana nyota, aka-

waambia, wakimwona mtoto warudi wampe habari zake zote, apate kwenda mwenyewe kumsujudia. Lakini maneno yake ya hila tu.

Walipotoka Yerusalemi wakaiona nyota, ikawatangulia hatta alipo mtoto. Wakiiona wakafurahiwa sana. Wakifika nyumbani wakamwona mtoto na Maryamu mamaye, wakamsujudia, wakafunua masanduku yao wakamletea tunu, thahabu, na uvumba, na manemane.

Tunu hizi zote za thamani. Thahabu ndiyo zawadi kwa wafalme, na uvumba huvukizwa katika dini ya Muungu, na manemane ndiyo dawa ya kuzuilia kuoza, iliyotumiwa katika kuwazika watu wakuu.

Herode akiwangoja Wamajusi katika Yerusalemi, Muungu akapeleka Malaika kwao, na kwa Yusuf, kuwaambia Wamajusi wasirudi kwa Herode, na kumwambia Yusuf amchukue mtoto akimbie upesi hatta Misri, atoke katika ufalme wa Herode.

Hivi Muungu akabatilisha hila ya mfalme aliyetaka kumua mtoto kwa uwivu. Hatta Herode asipopata habari za mtoto akaona hasira nyingi, akapeleka asikari akawaua watoto wote walioko katika Betlehemu wasiopita miaka miwili, akathani yakini atamua mtoto aliye Ma-

siya, illakini Muungu ametangulia kumponya. Watoto hawa waliouawa kwa ajili yake Masiya ndio tunaokumbuka killa mwaka siku ile ilioitwa, Siku zao wasio na hatiya.

SOMO VI.

Utoto wa Isa, Isa pamoja na Waalimu katika Hekalu.

(Matt. II. 19—23; Luk. II. 40—52.)

Isa hakukaa sana katika Misri. Herode alikufa baada ya siku chache. Alipokwisha kufa Warumi wakagawa ufalme wake kwa sehemu nne. Sehemu moja, Uyahudi na mji wake mkuu Yerusalemi ndio ufalme wa Arkhelao mwana wa Herode. Sehemu ngine Galilaya aliyopewa Herode Antipa mwana wa Herode mkuu. Ndiye Herode aliyetawala siku za Bwana wetu.

Alipokufa Herode mkuu Muungu akamwonya Yusuf arudi, akarudi, illakini akaogopa kwenda Betlehemu, akapita hatta Galilaya, akakaa mji wake wa zamani, Nazareti.

Yusuf alitenda kazi, na kazi yake kuwa sermala. Isa akakaa nyumbani mwake akamtii yeye na Maryamu mamaye, akatenda kazi mwenyewe. Tumeambiwa ya kwamba mtoto

akakua, akapata nguvu rohoni, akajaa hekima, na neema ya Muungu juu yake.

Hatta alipopata miaka thenashara akaanza kwenda Yerusalemi kwa siku kuu ya Pasaka pamoja na wazee wake. Ndiyo sheria ya Wayahudi killa mtu aende Yerusalemi marra nne killa mwaka kumwabudu Muungu hekaluni, naye mtoto akipata miaka thenashara walimthania kijana, wala si mtoto tena.

Akaenda Yerusalemi pamoja na Maryamu na Yusuf, wakatenda killa iliyowapasa, wakarudi. Hatta wahpotoka Yerusalemi hawakumwona Isa, wakathani, Hana buddi kuwa pamoja na jamaa na majirani yetu. Hatta jioni wakimtafuta hawakupata kumwona, wakaogopa sana wakiona kama amepotea, wakarudi Yerusalemi wakimtafuta.

Hatta siku ya tatu wakamwona, amekaa katika hekalu pamoja na waalimu akiwasikia na kuwauliza, watu wote waliosikia wakataajabu kwa akili zake na majibu yake.

Maryamu alipomwona akashangaa, akaena, Mwanangu, mbona umetutendea hivi, baba wako na mimi tumekutafuta kwa huzuni. Akawaambia, Ginsi gani kunitafuta, hamkujua sina buddi kuwa kwa Baba yangu. Kwa Baba

wake ndiyo kwa mambo ya Muungu, na katika nyumba ya Muungu aliye Baba wake, lakini hawakutambua maneno haya.

Akafuatana nao hatta Nazareti akawatii. Illa mama wake aliyejua ginsi alivyozaliwa, akakumbuka maneno yake, akayafikiri moyoni akingoja wakati yatakapoelea pia. Akakaa miaka mingi hatta Yusuf amekufa, wala hatuna habari za miaka hii, isipokuwa tumeambiwa ya kwamba, Isa alizidi katika hekima na uzima, na kupendeza Muungu na watu.

SOMO VII.

Kuhubiri Yohanna mbatizaji.

(Matt. III. 1—6; Mark. I. 4—6; Luk. III. 1—11; Yoh. 1. 6—8)

Yohanna alikaa hatta alipopata miaka thelathini asionekane sana na watu. Babaye na mamaye walikuwa wazee, labuda wamekufa zamani, nayee alikaa nyikani, kama Eliya, akivaa nguo za nyikani, akila chakula cha nyikani, hakupenda wala mavazi meroro, wala chakula kitamu, alikuwa akimkumbuka Muungu tu.

Kwa Wayahudi mtu alithaniwa kijana tu hatta alipopata miaka thelathini, ndipo alipokuwa mtu mzima. Basi Yohanna akiwa mzima

Muungu akamwita kwa kazi yake, akaja kwa watu mpakani mwa unyika akawahubiri ya kuwa ufalme wa Muungu umekaribia, sharti watubu katika maovu yao yote, wasikatike na Muungu. Nao waliosikia akawabatiza kwa maji. Kutia maji ndiyo ishara ya kusafisha. Mtu akitaka kuwa safi hujitia maji. Hivi kwa ishara ya kutubu watu wakamtaka Yohanna awatie maji, akawatia. Kwa hiyo akaitwa Yohanna Mbatizaji, maana yake, atiaye maji. Palikuwa na Yohanna wa pili, mwana wa Zebedayo, aliyeitwa Yohanna Mwanjilisti, kwa sababu ndiyo aliyeandika Anjili.

Kazi yake Yohanna Mbatizaji ndiyo kumtangulia Masiya na kuwaonya watu wajiweka tayari wapate kumkaribisha. Kama alivyosema nabii Isaya, Sauti yake aliaye nyikani, Tengenezeni njia ya Yahuwa, nyosheni mapito yake. Killa boonde litajalizwa, na killa mlima na kilima kitashushwa, yaliyopotoka yatanyoshwa. na yaliyoparuza yatalainishwa, na wenyi mwili wote wataona wokovu wa Muungu. Ndiyo dasturi, mfalme akitaka kusafiri, kupeleka watu mbele yake wazitengeneze njia. Hivi Masiya akija duniani manabii wamepelekwa mbele yake kutengeneza njia, maana yake kugeuza watu

katika maovu yao, wasiharibike na kuja kwake. Naye Yohanna aliye karibu mbele yake amekwitwa tena Mtangulia.

Yohanna akihubiri, watu wengi wakatoka wabatizwe naye, Yohanna akawaambia hawana budi kutubu na kutoa mazao ya toba, ndiyo matendo mema. Wayahudi waliona kiburi nyingi kwa sababu ya kuwa watoto wa Ibrahimu, aliye rafiki wa Muungu, Yohanna akawaambia, Msiseme moyoni, Ibrahimu ndiye baba wetu, kwa sababu Muungu aweza hatta katika mawe haya kumfanyia watoto Ibrahimu. Maana yake, watoto wa Ibrahimu machoni pa Muungu ndio walio na imani kama Ibrahimu, sio waliozaliwa naye, wasipokuwa na imani. Hatta wageni wakiwa na imani wamefanana na Ibrahimu kuliko watoto wake wa mwilini. Wakimwuliza, Tufanyeje tena? Akawaambia, Killa mwenyi chakula ampe asiyenacho, na killa mwenyi nguo ampe asiyenayo.

SOMO VIII.

Watu waliokuja kwa Yohanna Mbatizaji.

Matt. III. 7—12; Mark. I. 7—8; Luk. III. 11—14.

Watu wa inchi wakaja wengi kumsikia Yohanna. Wangine wakatubu kwa kweli, wa-

ngine wakaenda zao, wakasahau maneno yake. Illakini killa mtu amefundishwa kazi yake.

Wakaja asikari waliofuata Kaisari wa Rumi, ao wafalme walio chini yake, waliotharau watu wa inchi wakawatendea vibaya vingi. Yohanna akawaambia, Msitendee mtu jeuri, wala msimstaki mtu burre, wala msitake kitu illa mshahara wenu tu.

Wakaja na Mapublikano, ndio watu walionunua kwa Warumi ushuru na kodi. Hulipa Kaisari fetha kwa jumla, halafu wakatwaa kodi na ushuru. Hawa walikuwa na nguvu nyingi na dasturi yao kutwaa zayidi ya haki, na watu waliokataa kulipa wakawastaki kwa Warumi wakawauthi sana. Wayahudi hawakupenda kabisa kulipa kodi kwa wageni, kama Warumi, Mapublikano wakachukiwa sana nao. Yohanna akawaambia, Msitwae illa iliyo haki yenu.

Wakaja na Masadukayo, ndio watu wa elimu waliosema kama hapana kiyama wala malaika wakafikiri mambo ya duniani tu. Walisema ya kuwa Muungu amewapa watu wake inchi, na afia, na mali, bassi. Hawa walikuwa watu wakuu na wenyi mali, ndio waliomchukia wakamfukuza sana Bwana wetu na waanafunzi

wako. Wakohani wakuu wa siku zile wakafuata mathehebu ya Masadukayo.

Wakaja tena Mafarisayo, ndio adui zao Masadukayo, wakawaona kama makafiri. Mafarisayo walishika sana sheria ya Muungu, wakafuata tena dasturi za wazee wao. Walifunga, wakasali sana, wakatoa sehemu ya kumi ya killa kitu walicho nacho, hatta ya mboga, illakini kwa ndani hawakujitunza sana, walikuwa na kiburi, wakapenda kusifiwa na watu, wakafanya hila, wakapenda mno kupata fetha. Kwa sababu hiyo Bwana wetu akawalaumu sana kwa unafiki wao. Mnafiki ndiye ajifanyaye kwa watu mwema sana, asipokuwa mwema moyoni.

Yohanna akiwaona Masadukayo na Mafarisayo wakija kwake, akashangaa, kwa sababu ameona wanataka heshima kwa watu, wala hawakunenyekea kwa sababu ya thambi zao. Akawakaripia, Enyi waana wa nyoka, ni nani aliyewaonya mkimbie ghathabu ijayo. Hatta na ninyi mtoe mazao ya toba.

Watu walio maskini na wanenyekevu aliwatuliza, watu wa mali na wenyi kiburi akawanenea ukali.

SOMO IX.

Wajumbe wapelekwa kwa Mbatizaji kumwuliza, Nani wee?

Luk. III. 15—18; Yoh. I. 15—28.

Hatta wakuu wa Yerusalemi wakiona watu wote wanamfuata Yohanna, wakapeleka wajumbe kumwuliza, Nani wewe, wapate kusikia kama ajifanya nabii, ao labuda Masiya mwenyewe.

Wakapeleka Wakohani na Walawi. Walawi ndio watu wa kabila ya Lawi, ndiyo kabila ya Musa na Haruni. Kabila hiyo haikupewa sehemu katika inchi ya Kanaani kwa sababu kazi yao kungoja hekaluni mwa Muungu, na urithi wao sadaka na thabihu za watu. Katika kabila hiyo watoto wa Haruni wakachaguliwa kuwa Wakohani, ndio waliotoa thabihu, na sadaka, na haja za watu mbele ya Muungu, wakavukiza uvumba kwa heshima yake. Wakohani ndiyo walioingia katika patakatifu pa Muungu wala hakuna watu wangineo, hatta Walawi, wasio wazao wa Haruni waliopewa ruksa waingie humo.

Bassi wajumbe hawa Wakohani na Walawi wakaja kwa Yohanna, wakamwuliza, Nani we-

ye? Ndiwe Masiya? Akajibu, Siye.

Nabii Malaki alinena ya kwamba Muungu atampeleka Eliya mbele ya Masiya. Ndiyo mfano wa Yohanna aliyekaa nyikani, akavaa nguo za nyikani, akatoa kwa nguvu maneno ya kuonya kama Eliya. Wayahudi walithani ya kwamba Eliya mwenyewe atarudi, wakamwuliza Yohanna, Ndiwe Eliya? Akanena, Siye.

Musa aliwaambia Waisraeli, Yahuwa Muungu wenu atawaletea Nabii kama mimi, msikilizeni. Wakamwuliza Yohanna, Ndiwe nabii yule? Akajibu, Siye.

Hivi Yohanna akakataa kupewa majina yote ya heshima. Wakashangaa, wakanena, Nani weye, tuambie, usemaje mwenyewe, tupate kuwajibu waliotupeleka. Akanena, Mimi, sauti yake aliaye katika nyika, nyosheni njia ya Yahuwa, kama alivyosema nabii Isaya. Angalia unenyekevu wake, mimi si mtu, mimi sauti tu.

Katika wajumbe walikuwa Mafarisayo, waliopenda sana sheria na utaratibu, wakamwambia, Kama wewe si Masiya, wala si Eliya, wala si Nabii yule, illa sauti tu, mbona kubatiza watu?

Akanena, Ubatizo wangu, ni ubatizo wa kutangulia tu, na ku'mwekea tayari afuataye. Ndiye aliye mkuu, sistahili mimi wala kufungua, wala kuchukua viatu vyake. Nabatiza kwa maji, yee atabatiza kwa moto na kwa Roho Mtakatifu. Mimi nahubiri kuja kwake, yee akija atawapambanua wema na wabaya, atawakusanya walio wema ghalani mwake, ndio mbinguni, atawafukuza wasio wema wakae motoni.

SOMO X.

Ubatizo wa Bwana wetu.

Matt. 3—13; Mark. 1—9; Luk. 3—21; Yoh. 1—33.

Bwana wetu Isa Masiya alizaliwa miezi sita baada ya Yohanna wa Zakariya Mbatizaji. Akipata miaka thelathini akaanza na yeye kazi yake, akaja kwanza kwa Yohanna abatizwe pamoja na watu.

Yohanna amemjua tangu utoto akamjua hana thambi, akamkataza akanena, Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe wanijia mimi?

Isa akamwambia, Uache sasa kwani ndivyo ilivyotupasa kutimiza haki yote. Alipenda kujifanya kabisa kama sisi, tupate kufuata namna yake.

Yohanna akambatiza, hatta marra akitoka majini mbingu zikamfunukia, akaona Roho ya Muungu ikimshukia kama hua, ikimtulilia, na sauti katika mbingu kunena, Huyu mwanangu mpendwa, anipendezaye. Ndiyo ishara aliyoambiwa Yohanna ataona kumwonyesha aliye Masiya. Hatta saa ile hakumjua, baadaye akamwonyesha kwa waanafunzi wake kama ndiye aondoaye thambi za watu.

SOMO XI.

Jaribu la Bwana wetu Isa.

Matt. IV. 1—11; Luk. IV. 1—13.

Bwana wetu alikuwa mtu halisi. Killa mtu hujaribiwa na Shetani, hatta Bwana wetu akajaribiwa naye, illa hakushindwa.

Alipokwisha kubatizwa akaenda nyikani, mahali pasipo watu, akakaa huko siku arobaini mchana na usiku akifunga na kuomba. Hatta akiona njaa, shetani akajaribu kumshawishi asifunge tena. Akamwambia, Ukiwa mwana wa Muungu uamuru mawe haya kuwa mikate. Isa akamjibu, Imeandikwa, Mtu haishi kwa chakula tu, illa kwa killa neno litokalo kanwani mwa Muungu. Maneno haya maneno ya

Musa (Deut. VIII. 3) aliyesema ya kwamba Muungu amewalisha Waisraeli katika jangwa kwa chakula kilichotoka mbinguni, wapate kujua ya kwamba neno la Muungu lamfaa mtu marra nyingi kuliko chakula.

Shetani akamchukua hatta Yerusalemi aka-'mweka juu ya mnara wa hekalu. Akamwambia, Ukiwa mwana wa Muungu, ujitupe chini, kwani imeandikwa, Atakuagizia malaika zake, na mikononi mwao watakuchukua usijikwae mguu jiweni. Isa akamjibu, Imeandikwa tena, Usimjaribu Yahuwa Muungu wako. Tukiingia hatarini katika kufuata amri za Muungu atatulinda, tukijitia hatarini burre ndiyo kumjaribu.

Tena shetani akamtwaa aka'mweka juu ya mlima mrefu sana, akamwonyesha ufalme wote wa duniani na utukufu wao, akamwambia, Haya yote nitakupa, ukiniangukia unisujudie. Isa akamwambia, Ondoka hapo, shetani, kwani imeandikwa, Umsujudie Yahuwa Muungu wako naye peke yake umtumikie.

Shetani akamwacha, wakaja malaika wakamngojea.

Hivi Bwana amejaribiwa kwa njaa na tamaa za mwili, na tena kwa kiburi na kujisifu kwa ajili ya kupendwa na Muungu, na tena kwa

tamaa za mali, na nguvu, na ukuu wa duniani, akayashinda majaribu yote.

SOMO XII.

Wafuasi wa kwanza wa Isa.

Yoh. I. 29—49.

Isa akarudi katika nyika, akaanza kufundisha. Mwanzo akajikusanyia watu wema waliojua Maandiko Matakatifu, wakamtazamia Masiya. Yohanna Mbatizaji akawaambia waanafunzi wake ya kuwa Isa ndiye iliyompasa kuja kuondoa thambi za ulimwengu. Alikuwa akitembea na Andrea na mtu mwingine aliye mwanafunzi wake, wakamwona Isa, Yohanna akawaambia, Tazama Mwana kondoo wa Muungu. Maana yake, aliyetolewa kwa ajili ya thambi za watu, kama killa siku hekaluni hutoa mwana kondoo kwa thabihu, na katika Pasaka damu ya mwana kondoo ndiyo iliyowalinda Waisraeli, Wamisri walipokufa.

Waanafunzi wale wawili waliomsikia wakamfuata Isa. Akawauliza, Mwataka nini? Wakamwambia, Bwana, wakaa wapi? Akawaambia, Njooni mwone. Wakaenda, wakakaa naye siku ile.

Halafu Andrea akaenda kumtafuta Simau nduguye, akamwambia, Tumemwona Masiya. Akamleta kwa Isa. Hatta alipomwona, akamwambia, Ndiwe Simau wa Yona utaitwa Kefa, maana yake, jiwe. Kefa ni neno la Kiyahudi, na Petro ni neno la Kiyonani, na maana yao moja, ndiyo jiwe.

Isa akamwona Filipo, akamwambia, Nifuate. Filipo alikuwa jirani wao Andrea na Petro na mji wao jina lake Betsaida. Filipo akamtafuta Natanael, akamwambia, Tumemwona aliyeandikiwa na Musa na manabii, ndiye Isa wa Nazareti mwana wa Yusuf. Natanael akamwambia, Kipataje kitu chema kutoka katika Nazareti? Akamwambia, Njoo uone. Sifa za Nazareti si njema, na kumwita Bwana wetu Mnazareti ni kama kumshutumu.

Illakini Natanael akaenda, hatta Isa alipomwona akanena, Tazama Mwisraeli wa kweli, asiye na hila. Natanael akamwambia, Wanijuaje? Isa akamwambia, Mbele Filipo asijakuita, ulipokuwako chini ya mtini nalikuona. Natanael akamjibu, akanena, Bwana wangu ndiwe Mwana wa Mungu, ndiwe Mfalme wa Israeli.

SOMO XIII.

'Kufungwa na kuuawa Yohanna Mbatizaji.

Matt. XIV. 1—12; Mark. VI. 14—29;
Luk. III. 19—20 IX. 7—9.

Yohanua Mbatizaji hakuacha kuhubiri kwake alipokuja Isa, illa hakudumu sana, kwani kazi yake Yohanna kutengeneza njia ya Bwana wetu, ikampasa kupunguka, Bwana wetu akizidi. Yohanua akaondolewa katika kazi yake na Herode, mfalme wa Galilaya.

Herode alitaka kumwoa Herodiade mke wa nduguye Filipo, Yohanna akamkataza, akasema, Si halali kuwa na mke wa nduguyo. Herode akapeleka asikari, akamkamata Yohanna akamtia gerezani, akamwoa Herodiade. Hakutaka kumua kwa sababu akamjua mtu mwema na mtakatifu, naye amesikia maneno yake kwa furaha.

Illa Herodiade akamchukia akataka sana kumulia mbali. Hatta Herode alipofanya karamu kuu kwa siku ya kuzaliwa kwake, akawaita watu wote walio wakuu wa Galilaya, akaja binti Herodiade akacheza mbele yao, akampendeza sana mfalme, hatta akamwapia, 'Takupa killa ulitakalo, hatta nuss ya ufalme.

Akamwuliza mamaye, Nitake nini ? Herodiade akamwambia, Utake kitwa cha Yohanna Mbatizaji katika kombe. Akaenda akamwambia mfalme, Ndilo nilitakalo. Herode akaona amenaswa, akajuta sana, illakini hakuthubutu kukataa. Akapeleka asikari wakamkata kitwa wakakileta, binti akapewa, akampa mamaye.

Waanafunzi wakaja wakatwaa mzoga, wakazika, wakaja wakamwambia Isa.

Herode alijua ya kwamba amefanya thulumu, hatta akisikia habari za matendo makuu aliyoyatenda Isa, moyo wake ukastuka, akanena, Ndiye Yohanna niliyemua, amefufuka katika wafu. Illakini Herode hakutubu, wala hakuacha maovu yake.

SOMO XIV.

Harusi kwa Kana ya Galilaya.

Yoh. III. 1—12.

Palikuwa harusi katika majirani ya Isa, akaitwa yeye na mama wake na waanafunzi wake. Wakaenda wakakaa kitako wakila na

kunywa. Hatta wakiisha kunywa kidogo mvinyo umekwisha. Mama wake Isa akamwambia, Hawana tena mvinyo. Akamwambia, Ngoja kwanza, wakati wangu haujawadia. Mama wake akawaambia watumishi, Killa awaambialo mfanye.

Palikuwako na makasiki sita ya maji, watu wapate kunawa mikono na kutakasa vitu kwa desturi ya Wayahudi, waliotumia maji sana wasiivunje sheria yao.

Isa akawaambia watumishi, Jalizeni makasiki, wakayajaliza. Akawaambia, Mteke, kamchukulia aliye mkuu wa karamu, wakachukua. Hatta akionja akaona yamekuwa mvinyo na mvinyo ulio mwema, hatta akamwambia bwana harusi, Mbona umeweka mvinyo ulio mwema hatta sasa ?

Hivi Bwana wetu akaonyesha na wema wake na nguvu zake. Amefuatana na majirani yake katika furaha zao, hatta akiona wamepunguka, akawapa waliohitaji na kuzidi, akawapa kwa nguvu zisizo za waana Adamu, kwani mtu gani awezaye kugeuza maji kuwa mvinyo ?

Waanafunzi wakazidi kumwamini wakiona ajabu aliyoitenda.

SOMO XV.

Isa kwa Nazareti.

Luk. IV. 16—30.

Alipokwisha kufungwa Yohanna, Isa akaja Galilaya akihubiri Ufalme wa Muungu, akinena, Wakati umewadia, ufalme wa Muungu u karibu, tubuni, mkaiamini Anjili.

Akaja kwa Nazareti alipokuwako mtoto, na kwa dasturi yake akaingia katika sunagogi siku ya sabato, akasimama asome.

Katika killa mji wa Wayahudi palikuwa mahali pa kukusanyika kusoma Torati ya Musa na Maandiko ya Manabii, na kuimba Zaburi, palipokwitwa Sunagogi, maana yake, kusanyiko. Hawakutoa thabihu, wala kufanya mambo ya siku kuu, illa katika hekalu la Yerusalemi. Kazi ya Sunagogi ndiyo kusoma na kuimba, na kuomba, na kufasiri Maandiko Matakatifu. Wakuu wa Sunagogi wakachagua watu kusoma, ao kunena maneno waliyo nayo.

Isa akisimama wakamletea kitabu cha Manabii, na sehemu aliyosoma, ndiyo ya Nabii Isaya, palipoandikwa, Roho ya Yahuwa juu yangu, kwani amenitia mafuta nihubiri Anjili kwa masikini, amenipeleka niwaponye wenyi

moyo uliovunjika, kuwahubiria wokovu waliofungwa, na kupata kuona kwa vipofu, kuwaweka huru waliochubuka, kuhubiri mwaka wa ukubali wa Yahuwa. Akafunga kitabu akampa mngoje, akakaa kitako. Kukaa kitako ndiyo ishara ya kwamba ana neno la kusema.

Hatta wote wakimtazama akaanza kuwaambia, Leo andiko hili limetimia masikioni mwenu. Kwani maneno haya ya nabii ndiyo maneno ya kumwonyesha Masiya. Wote wakaona kwa ajabu maneno ya neema yaliyotoka kanwani mwake.

Illakini hawakusikiliza, wakaona hasidi, wakinena, huyu mmoja wetu, mbona amejifanya mkuu? Mbona hafanyi hapa miujiza tupate kuona sisi? Wakanena, Siye huyu sermala? Wakaondoka wote wakaenda naye hatta kilimani, wakataka kumwangusha chini. Illa yeye hakuwaacha, akapita kati yao, akaenda zake.

SOMO XVI.

Mafundisho ya Bwana wetu.

Matt. V. 1—12; Luk. VI. 20—23.

Killa alikokwenda Bwana wetu watu wengi wakamfuata wapate kusikia maneno yake. A-

kawafundisha po pote, na njiani, na nyumbani, na pwani, na mlimani.

Katika sura za tanu, na sita, na saba ya Anjili ya Mattayo tunayo maneno mengi aliyowaambia.

Mwanzo yametiwa maneno ya heri, kuonya watu wasifikiri heri ya duniani tu. Watu wa dunia hii wanaona kuwa heri ndiyo kuwa na mali, na furaha, na heshima ya watu. Bwana wetu anasema ndio heri walio maskini, na huzunini, na wanaochukiwa na watu, kwani kuwa heri kwa kweli si jambo la duniani illa jambo la Muungu. Nao manabii wa zamani walifukuzwa na watu wa siku zao, illa manabii ya uwongo walisifiwa na watu.

Waisraeli walipewa sheria na Muungu. Bwana wetu asema, hakuja kuiharibu sheria, illa kutimiza. Bassi sheria yasema usiue, wala usizini. Bwana wetu anasema, Usiue, illakini usipoua hupendezi Muungu ukiwachukia ndugu zako, ukiwatukana, ukiona hasira nao burre. Na tena usizini, illakini kumpendeza Muungu usitamani mke asiye mke wako, wala hatta kutaka kumtazama. Katika sheria wameambiwa wapende jirani zao. Bwana wetu anatuambia tupende watu wote, hatta maadui yetu.

Watu husema, imempasa mtu kumtendea vema aliyemtenda mema kwanza. Bwana wetu asema, Utangulie kuwatendea vema wasiokupenda, wala wasiokufaa, kama Muungu anavyowatunza watu wote, hatta wabaya nao wasio na shukuru.

Atuambia tena katika mambo yetu yote kumkumbuka Muungu, wala si watu. Mtu akisali sana, akifunga sana, mtu akitoa mali mengi kwa sadaka husifiwa na watu. Bwana wetu atwambia, tuepuke sifa za watu. Afathali tusali kwa siri, tufunge kwa siri, tutoe sadaka kwa siri, tusisifiwe nao watu, hatta tusijisifu wenyewe. Ndipo tutakapopewa thawabu na Muungu. Tena tukiomba, tusinene maneno mengi, tusipojua maana yao, ao tusipofikiri. Akatoa namna ile ya kusali tunayoita, Sala ya Bwana wetu.

Hatta kwa mambo ya duniani, kama kupata chakula na nguo, atwambia, tusitaabike wala tusishughulike, illa tufanye killa siku kazi ya siku ile, tukimwamini Muungu kwa mambo ya kesho, wala tusitake kukusanya mali mengi hapa duniani, illa afthali tutake mali ya milele yaliyowekwa mbinguni, watakayopewa wampendezao Muungu.

Mwisho anena, haifai kukubali maneno yake, na kumwita Bwana, Bwana, tusipoyatenda tuliyoambiwa naye.

SOMO XVII.

Mitume thenashara.

Mark. III. 13—19; VI. 7—11; Luk. VI. 12—19; IX. 1—5 Matt. X. 2—13.

Watu wengi walimfuata Bwana wetu, wangine wakachukizwa wakamwacha, wangine wakamwacha kwa hofu ya adui zake, wangine wakakaa naye hatta mwisho. Katika hawa walio amini akachagua kumi na wawili kuwa karibu yake. Akawaita mitume, kwa sababu aliwatuma kwa kazi yake. Jina hili la mtume limetumiwa kwa Wayahudi, kuonyesha watu waliopelekwa na Mkohani mkuu kuamuru mambo ya dini katika Wayahudi wasiokaa Yerusalemi. Hivi Mkohani wetu mkuu, ndiye Isa Masiya, akapeleka mitume yake kutengeneza mambo ya dini katika kanisa lake. Hawa mitume wakachagua watu kutenda kazi yao wakifa wenyewe, na hivi hatta leo waalimu wa kanisani wamechaguliwa, wakatumwa na Askafu waliowafuata mitume.

Masiya akachagua watu thenashara, kwa namna ya makabila thenashara ya Wayahudi. Kwani kanisa lake Masiya ndilo lililo sasa taifa la Muungu. Kwanza, na wakohani na watu walifuata kwa uzazi wa mwilini, sasa hufuata kwa uzazi wa rohoni. Kwanza ufalme wa Daudi, ufalme wa duniani, sasa ufalme wa mwana wa Daudi, ndiye Isa Masiya, ni ufalme wa rohoni na ufalme wa mbinguni, wala sio wa duniani.

Katika hawa thenashara walikuwa watatu waliofuata sikuzote naye Masiya, hatta wasipo wangine. Ndiyo majina yao.

1. Siman, ndugu wa Andrea, yeye na ndugu yake walikuwa wavuvi wakavua samaki katika bahari, ao ziwa la Galilaya. Alikwitwa tena Baryona, maana yake, bin Yunus, ao mwana wa Yona. Isa akampa jina jipya ndilo Jiwe, kwani ndiyo maana ya jina lake Petro, ao Kefa. Petro aliandika nyaraka mbili tunazosoma hatta leo.

2. Yakobo, mwana wa Zebedayo, yeye na ndugu yake Yohana walikuwa wakitenda kazi ya kuvua samaki pamoja na baba wao walipoitwa na Isa, wakaacha mali yao yote wakamfuata. Yakobo ndiye mtume wa kwanza aliyekufa kwa ajili ya Bwana wake, akiuawa na

mfalme Herode (Matendo XII. 2.)

3. Yohana aliyeitwa Mwanjilisti, kuonyesha siye Mbatizaji, illa aliyeandika Anjili ya 'nne. Akaandika tena nyaraka tatu na kitabu cha Ufunuo, ulio mwisho wa msahafu.

Hawa ndugu wawili wakaitwa na Bwana wetu Boanerge, maana yake, Waana wa radi, kwa kuwa wepesi na wenyi nguvu.

Baada ya hawa walikuwa

4. Andrea, nduguye Simán.

5. Filipo wa Betsaida, ndio mji wa Andrea na Simán.

6. Bartolomayo, ao Natanael. Maana ya Bartolomayo ndiyo mwana wa Tolomayo.

7. Mattayo, ao Lawi, aliyekuwa mtoza ushuru. Ndiye aliyeandika Anjili ya kwanza.

8. Tomaso, aliyeitwa Didumo, ama mtoto wa pacha.

9. Yakobo wa Alfayo. Ameitwa Yakobo mdogo, kumpambanua na Yakobo wa Zebedayo aliyeitwa Yakobo mkubwa. Yakobo aliyekuwa ndugu wa Bwana wetu na Askafu wa kwanza wa Yerusalemi, naye aliyeandika Waraka wa Yakobo, labuda ndiye huyu.

10. Yuda, ao Taddayo, ao Lebbayo aliyeitwa Yuda wa Yakobo. Tunao waraka mmoja

alioandika. Naye Yuda aliitwa ndugu ya Bwana wetu.

11. Simán, aliyeitwa Zelote ao Kanani, maana yake 'mwivu. Palikuwa zamani zile Wayahudi walioitwa Mazeloti, kwa sababu ya kuwa na uwivu sana juu ya makafiri na Wayahudi wasioshika sana sheria ya Musa.

12. Yuda Iskariota, maana ya Iskariota ndiyo mtu wa Kariot, mji wa Wayahudi, ndiye aliyemtoa Isa kwa vipande thelathini vya fetha akawaonyesha maadui yake mahali alipo.

Hawa wathenashara Isa akawapeleka waende wawili wawili kuhubiri katika miji ya Uyahudi, akawapa nguvu juu ya pepo wabaya na kuponya ugonjwa. Wakatoka wakahubiri, watu watubu. Wakafukuza pepo, wakawatia mafuta walio wagonjwa, wakapona. Mitume wakakusanyika tena kwa Isa, wakamwambia mambo yote nayo waliyoyatenda, nayo waliyoyafundisha.

SOMO XVIII.

Mwanamke wa Samaria.

Yoh. IV. 1—24.

Samaria ndiyo inchi iliyo kati ya Uyahudi na

Galilaya. Kwanza Waefraimi walikaa humo, na Wafalme wa Israeli walijenga mji mkubwa ulioitwa Samaria. Wafalme wa Ninawi wakawashinda Waisraeli wakawachukua hatta Ninawi, wakaleta wageni wakawaweka katika inchi ya Samaria. Hivi watu wa Samaria si Wayahudi illa machanganyiko ya wageni walioletwa na Wafalme wa Ninawi, na masalia madogo ya Waisraeli, na watoro, na watu waliofukuzwa katika Yerusalemi. Palikuwa sikuzote vita na machukio kati ya Wayahudi na watu wa Samaria. Wasamaria wakajenga hekalu juu ya mlima Gerizim wakaabudu huko mahali pa Yerusalemi. Bwana wetu akipita katika inchi yao, akitaka kukaa usiku katika mji mmoja wao wakakataa, wakamfukuza kwa sababu alikuwa njiani kwenda Yerusalemi.

Isa akirudi katika Yerusalemi kwenda Galilaya, akafika kama aththuuri palipo kisima cha Yakobo, aliyempa mwanawe Yusuf. Akakaa kitako kisimani, waanafunzi wake wakaenda mjini kununua chakula. Hatta akikaa huko mwanamke wa Samaria akaja kuteka maji. Isa akamwambia, Nipe ninywe. Mwanamke akastaajabu, kwani Wayahudi waliona kunywa mkononi mwa Msamaria ndio unajisi. Aka-

mwambia, Ginsi gani Wee, Myahudi, wataka maji kwangu, niliye Msamaria?

Isa akajibu, Kama ungalijua ni nani akutakaye, nipe ninywe, ungalitaka kwake naye angalikupa maji yaliyo hayi. Mwanamke akamwambia, Bwana, kisima chaenda chini sana, wala huna cha kutekea, utapataje maji yale? Baba wetu Yakobo alitupa kisima hiki, akanywa maji yake, yeye na waanawe, na nyama zake, wewe u mkuu kuliko Yakobo? Isa akamwambia, Anywaye maji haya huona tena kiu, lakini anywaye maji nitakayompa haoni tena kiu, lakini atakuwa kama anacho kisima ndani yake kichemkacho kwa uzima wa milele. Mwanamke akamwambia, Bwana, nipe maji haya. Akamwambia, Mwita mume wako ukaje. Akamwambia, Sina mume. Isa akamwambia, Kweli umekuwa na waume watano na uliye naye sasa si mume wako, umesema kweli.

Mwanamke akaona ajabu ajue mambo yake, akamwambia, Bwana naona ndiwe nabii. Baba zetu waliabudu katika mlima huu, na ninyi mwasema imepasa watu kuabudu katika Yerusalemi. Isa akamwambia, Wokovu ni wa Wayahudi, ninyi hamjui mnayemwabudu, illakini saa inakuja, waabuduo wasiabudu wala katika

mlima huu wala katika Yerusalemi, illa waabuduo wa kweli watamwabudu Baba kwa roho. Muungu ni Roho, nao wamwabuduo hawana buddi kumwabudu kwa roho na kweli.

Mwanamke akamwambia, Najua ya kwamba akija Masiya, atatuambia mambo yote. Akamwambia Isa, Mimi nisemaye nawe ndiye.

Mwanamke akaenda mjini akawaita waume akinena, Njooni kamtazameni mtu aliyeniambia yote niliyoyatenda. Wakaja wakasikia, wakamtaka akae nao wapate kuzidi kumsikia.

SOMO XIX.

Masiya awabariki watoto.

Matt. XIX. 13—15; Mark. X. 13—16; Luk. XVII. 15—17.

Bwana wetu alipenda sana watoto. Mama wao walipowaleta kwake, akawakubali, akawatwaa mikononi, akawakumbatia, akawabariki. Hatta waanafunzi wake walipowakataza watu wasilete watoto kumuthi, akawakemea, akawaambia, Wacheni watoto wadogo waje kwangu, kwani wa kama hawa ni ufalme wa Muungu. Amin, nawaambia asiyepokea ufalme wa Muungu kama mtoto mdogo, hataingia

humo. Maana yake mtu akijivuna, akijiona mkuu, asipokubali kufundishwa kama mtoto mdogo hawezi kumpendeza Muungu.

Tena walipogombana waanafunzi wao kwa wao, killa mtu akitaka kuwa mkuu wa wote, Isa akatwaa mtoto aka'mweka kati, akawaambia, wakitaka kweli kuwa wakuu, wanenyekee, wajione kama mtoto yule aliye mdogo, kati yao, walio watu wazima na wazee.

Alionya watu tena wajilinde mbele ya watoto, wasiwafundishe mabaya, kwani amesema Muungu atamhukumia kwa ukali sana atakayepoteza mtoto. Kwani Muungu anapenda sana watoto, na malaika zao sikuzote karibu yake.

SOMO XX.

Miujiza ya Bwana wetu Isa Masiya.

Bwana wetu akiona watu walioumia kwa ugonjwa, akawasikitikia, akawasayidia. Ndio mfano wetu killa tuonapo mtu aliyeteswa, tumsayidie kwa kadiri ya nguvu zetu. Illa Bwana wetu anayo nguvu za Muungu, naye akisema neno marra hufanyika. Hivi wakamletea wagonjwa, akawaponya. Dasturi yake kuwatia mkono, marra ugonjwa ukatoka. Illa-

kini watu wasiomwamini hawakupona. Wangine hawakuja kwake, wangine hawakumkubali. Akiwa katika Nazareti mji wake yeye, hakutenda miujiza mingi kwa sababu hawakumwamini.

Kulikuwa ugonjwa mmoja, ndio ukoma, usioponyeka kwa dawa, na watu wenyi ukoma wakafukuzwa katika miji yao, wakakaa 'nje, wala watu hawakuthubutu kuwakaribia wasiambatizwe na ugonjwa. Illa Bwana wetu akimwona mtu mmoja mwenyi ukoma aliyekuja kwake akampigia magote akimsihi sana kwa imani, akatoa mkono akamgusa, akafukuza ukoma kwa mkono wake, mtu akapona marra moja. Ubaya wo wote hauwezi kumshika Bwana wetu, wala kukaa mbele yake.

Mwanamke mmoja aliye mgonjwa akamfuata Bwana wetu katika makutano, akagusa nguo zake kwa imani, marra akapona.

Illakini neno lake Isa latosha pasipo kuja ao kuwaona wagonjwa. Mtu mmoja mkuu akimsihi sana aje aponye mwana wake, akamwambia, Nenda zako, mwanawo amepona. Akasadiki neno lake, akarudi, hatta akifika nyumbani akaona mwanawe amekwisha pona tangu saa ileile, alipomwambia Isa.

Mtu 'mmoja; aliye asikari Mrumi, akamwambia Bwana wetu, Mimi sistahili uje kwangu, sema neno tu, na mtu wangu atapona. Isa akamsifu sana kwa sababu yeye aliyekuwa mgeni, wala si Myahudi, kwa asili yake kafiri, amewapita watu wote waliomjua Muungu tangu utoto.

Bwana wetu akiwa katika sunagogi akaona mtu mmoja mwenyi mkono yabis, akamwambia, Unyoshe mkono wako, marra ukapona, akaunyosha, ukawa kama ule wa pili. Siku ya pili akaona mwanamke aliyeinamishwa wala hawezi kujinyosha. Akamwambia tu, akapona.

Marra nyingi akawaponya walio vilema, na vijiguu, na viziwi, na vipofu, nao waliopagawa na pepo, mashetani wakamjua wakamungama kama ndiye Mtakatifu wa Muungu. Illa watu hawakufikiri, wakamwona kama mtabibu tu. Hatta wakakataza watu wasitake kuponyeshwa siku ya sabato, kama ingalikuwa kazi yake Bwana wetu kuponya watu tu. Illakini kutenda kazi ya rehema na mapenzi ni siku zote halali. Akawauliza, mtu gani asiyelisha nyama zake siku ya sabato, ao akimwona ameanguka shimoni asiyemtoa. Si afathali nimfungue mwana wa Ibrahimu huyu aliyefungwa na She-

tani miaka hii mingi? Walu Yeye si kama mtabibu afanyaye dawa kusudi apate fetha, illa pasipo fayida yake, akawatendea watu vema.

SOMO XXI.

Isa atulize bahari na kutembea juu yake.

Matt. VIII. 23—27; Mark. IV. 37—41; Luk. VIII. 22—25; Matt. XIV. 24—33; Mark. VI. 47—51; Yoh. VI. 17—21.

Bwana wetu alikuwa akivuka ziwa la Galilaya katika chombo, naye amechoka akalala usingizi. Marra ikaja thóruba na pepo nyingi juu ya ziwa, mawimbi yakapiga chombo hatta wakaogopa yakini watapotea. Waanafunzi wake wakaja wakamwamsha, wakinena, Bwana, Bwana, tumekufa. Naye akiamka akasimama akazikemea pepo na mawimbi zikatulia. Akawaambia waanafunzi wake, I wapi imani yenu? Kama wangalikuwa na imani hawangaliogopa mno akiwapo yee.

Watu wote walioona wakastaajabu, wakanena, Mtu gani huyu, hatta bahari na pepo zamtii!

Marra ya pili, Isa amewapeleka waanafunzi wavuke chomboni, akakaa pwani mwenyewe. Hatta usiku walitaabika sana na upepo na ma-

wimbi, wakavuta sana wasiwezo kufika, marra wakamwona Isa anakuja akitembea juu ya maji. Wakapiga kelele kwa hofu, kwani wakathani udicho kivuli chake.

Akawaambia, Msiogope, ndimi nijaye. Hatta Petro akisikia, akajibu, akinena, Kama ndiwe, uniambie mimi nije kwako. Akamwambia, Njoo. Petro akashuka akaenda kidogo juu ya maji, illa akiona mawimbi, akaogopa, marra akaanza kuzama. Akamwitia Isa, Ee Bwana, uniokoe. Isa akampa mkono akamleta chomboni. Akamwambia, Ewe wa imani haba, mbona umeona shaka?

Marra akifika chomboni pepo zikatulia, wakafika upesi waendako.

SOMO XXII.

Isa alisha watu nyikani.

Matt. XIV. 13—21; Mark. VI. 31—44; Luk. IX. 10—17; Yoh. VI. 5—14; Mark. VIII. 1—9; Mark. XV, 32—38.

Shetani akitaka kumshawishi Bwana wetu ajilishe mwenyewe katika nyika akakataa. Illakini akiona watu waliokuja wamsikie wanakaa nyikani pasipo chakula, akatoa nguvu zake akawafanyia chakula.

Siku moja alipotaka Bwana wetu kukaa faragha akaenda nyikani kwa siri. Hatta watu waliposikia wakamfuata katika miji, hatta akaona watu wengi wanaomjia. Akawasikitikia akawaponya wagonjwa, akasema nao maneno ya Anjili. Hatta alasiri ikipita, waanafunzi wake wakamwambia, Hapa nyikani, na hatta sasa jioni, afathali uagane na watu waende zao, wapate kula. Isa akawaambia, Hawana amri kwenda zao, 'mwape chakula. Akamwambia Filipo; Tupate wapi chakula tuwape hawa? Filipo akaona haiyamkini, akamwambia, chakula cha dinari miteen hakingaliwatosha hatta kumpa killa mtu kidogo. Andrea akanena, Yupo hapa kijana mwenyi mikate mitano ya shayiri na visamaki vichache, illakini vitawafaa nini hawa wengi?

Isa akanena, Waambie watu wakae kitako. Wakakaa kitako hamsini kwa hamsini. Akaitwaa mikate akashukuru akagawanya kwa waanafunzi, na waanafunzi kwa watu, na samaki vivyo, hatta wakashiba wote.

Hatta wakiisha kula, akawaambia waanafunzi, Kusanyeni na makombo yaliyosalia, kitu kisipotee. Wakakusanya wakajaliza vikapo thenashara kwa makombo yaliyosalia. Nao

waliokula walikuwa kama elfu tano.

Baada ya haya ndipo alipowaambia waanafunzi wake wasitaabike kwa chakula kipoteacho, illa kwa chakula kiishipo kwa maisha ya milele, ndicho cha rohoni.

Marra ya pili alipokuwa karibu na ziwa la Galilaya akaona watu wengi sana wanamjia wakileta kwake wagonjwa, na vipofu, na viziwi, na wangineo wengi. Akawaponya, watu wakastaajabu wakiona wabubu wakinena, vilema wamepona, vijiguu wakienda, vipofu wakiona, wakamsifu Muungu.

Isa akawaita waanafunzi akawaambia, Nawasikitikia watu hawa wengi, kwa sababu wamekuwapo nami siku tatu wala hawana chakula.

Waanafunzi wakamwambia, Tupateje chakula cha kuwatosha watu hawa wengi mno hapa nyikani?

Isa akawaambia, Mikate mingapi mliyo nayo? Wakamwambia, Saba. Akawaambia, Watu wakae kitako. Akatwaa, akashukuru, akavunja, akawapa waanafunzi, waanafunzi wakagawanya kwa watu. Wakala wote, wakashiba, wakasaza iliyovunjika hatta kujaliza vikapo saba. Nao waliokula kama elfu nne.

SOMO XXIII.

Bwana wetu awaponya walioombewa kwake, naye asamehe thambi.

Luk. XVII. 16; Mark. VII. 24—30; Matt. IX. 2—7; Mark. II. 1—12; Luk. V, 18—25; Luk VII 36—50.

Bwana wetu alitembea katika inchi ya Israeli akafanya miujiza yake kwa Waisraeli, kwa sababu ndio walio waana wa ufalme. Illakini akawasayidia wachache wasio Waisraeli walio na imani sana. Kama watu kumi walio na ukoma, aliowaponya, mmoja wao alikuwa Msamaria, na siku moja alipopita karibu na Turo mwanamke wa inchi ile asiye Myahudi akaja kwake akamsihi sana aponye binti yake.

Kwanza hakusikiliza kwa sababu watu wale makafiri, illakini akimsihi sana na kwa unenyekevu mwingi, akamponya binti, kwa ajili ya imani ya mama yake, aliyemwombea.

Palikuwa tena mtu mwenyi kupooza aliyeletwa kwake na marafiki yake, alipokuwa nyumbani na watu wengi wamekaa ndani, na mlangoni, na 'nje. Wakataka kuingia, wasiweze, kwa watu kwa kuwa wengi. Illakini hawakurudi, wala hawakunena, hatuwezi bass. Wakafanya shauri wakapanda juu, wakafunua paa

wakamshusha rafiki yao mbele ya Isa.

Akaona Bwana wetu ginsi walivyompenda ugonjwa, na ginsi walivyotaka mno apone, akamwambia, Mwanangu, usione huzuni, thambi zako zimesamehoka. Ndio kumpa zayidi ya haja yake. Wale walitaka apone mwili, Bwana akamponyesha roho. Dasturi yetu kuwasikitikia na kuwalilia wagonjwa, illakini ugonjwa wa roho mzito kuliko ugonjwa wa mwili, na ugonjwa huu ndio thambi. Kama mtu akija kwa mtabibu kwa ajili ya ugonjwa hafifu, nayo akintazama anaona ya kuwa anao ugonjwa mgineo, asioujua, mzito na kufisha, hivi Bwana wetu wakaona watu, waliokuja kwake kwa sababu ya ugonjwa upitao, walikuwa na ugonjwa wa kuwaua milele, wasioukumbuka, wala wasioujua. Ndiyo kazi yake kuponyesha ugonjwa ulio mkuu.

Watu waliokaa huko, na waalimu na wazee, wakisikia maneno yake wakasema, Nani huyu? Kusamehe thambi kazi ya Muungu, si kazi ya mwana Adamu. Hawakufikiri ya kwamba mwana Adamu hawezi kuponya wagonjwa kwa neno lake tu, walithani, kuponya wagonjwa ni kazi ya mtabibu, na huyu mtabibu mkuu.

Illa Bwana wetu amenena makusudi awao-

nyeshe walivyokosa. Akawauliza, Ipi nyepesi, kuponya [ugonjwa marra moja ao kusamehe thambi, ipi iliyo kazi ya mwana Adamu, si yote kazi ya Muungu? Akamwambia, Ondoka, chukua kitanda chako, makusudi awaonyeshe ya kwamba anazo nguvu za Muungu.

Siku ya pili Bwana wetu alikuwa akikaa kitako kula nyumbani mwa Mfarisayo mmoja aliye mtu mkuu. Akaja mwanamke aliye na thambi nyingi, akalia miguuni pake kwa machozi mengi akambusu miguu. Mfarisayo amemjua, si mtu mwema kabisa, akaona moyoni, Kama angalimjua huyu angalimfukuza, kama hamjui huyu si nabii. Isa akaona mawazo yake kwa jicho la Muungu, akamwambia, Nina neno nataka kukuuliza. Akamwambia, Mwalimu, useme. Akamwambia, Palikuwa mtu aliyewawia watu wawili, mmoja fetha nyingi, wa pili fetha chache, akaona hawana kitu akawasamehe wote. Yupi atakayempenda sana? Akamwambia, Nathani aliyesamehewa nyingi. Bwana wetu akamwambia, Tazama mwanamke huyu, ginsi alivyonifanyia heshima, amekupita wewe marra nyingi. Kwa nini? Kwa sababu thambi zake nyingi kupita zako. Thambi ni deni kwa Muungu asiyoweza mtu kulipa wala

wewe, wala yeye. Thambi zako zilizo nyingi zimesamehekа kwa hiyo apenda sana, na zako si nyingi kwa hiyo amekupita. Akamwambia mwanamke, Nenda zako kwa amani, zimesamehewa thambi zako, imani yako nyingi.

Wote wakashangaa, wameona miujiza mingi, illakini maneno haya, ndiyo ya Muungu.

SOMO XXIV.

BWANA WETU ISA MASIYA AWAFUFUA WAFU.

Luk. VII. 11—16. VIII. 41, 45. Math. XVIII. 25. Mark V. 22—42. Yoh. XI. 1—45.

Imesalia miujiza iliyopita ile ya kuwaponya wagonjwa, ndiyo ya kufufua watu waliokwisha kufa.

Bwana wetu alikuwa siku moja akipita karibu na mji mdogo ulioitwa Nain. Hatta akifika mlangoni pa mji akakuta watu waliochukua mtu aliyekufa wamzike.

Watu wengi walikuwa wakifuata, kwa sababu aliyekufa alikuwa mtoto wa pekee wa mama yake, naye amefiwa na mumeo, watu wakamsikitikia. Bwana wetu akimwona, akamwambia, Usilie, kwani na yeye akamsikitikia. Akaja akatia mkono wake juu ya jeneza, waliochukua wakasimama. Akamwambia aliye-

kufa, Kijana, nakwambia, ondoka. Marra moja akajiinua akaanza kunena. Isa akamtoa kwa mamaye.

Watu wote wakashangaa, wakaona hofu, wakinena, Nabii mkuu ametutokea, Muungu amekuja kwa watu wake.

Palikuwa na mtu mkuu jina lake Yairo, naye alikuja kwa Isa kumwombea binti yake, aliyekuwa hawezi sana, wakamthania hana buddi kufa, akanena, hatta sasa amekufa.

Isa akaondoka akamfuata, watu wengi wakafuatana nao. Hatta njiani, watu wa nyumbani wakawakuta, wakanena, Binti amekwisha kufa, haifai kumleta Mwalimu. Illakini Isa akamwambia, Usiogope, uamini tu. Wakafika nyumbani.

Hatta wakifika wakaona watu waliolia, wakafanya maombolezo mengi. Isa akawaambia, Nyamazeni, kwani binti hakufa, amelala tu. Wakajua ya kwamba amekufa kabisa, wakacheka. Akawatoa wote, akatwaa Petro, na Yakobo, na Yohana, na wazee wa kijana, akaingia panapo kijana, akamtwaa mkono akamwambia, Talitha kumi, maana yake, Binti ondoka, akasimama. Akawaambia wazee wampe chakula. Alikuwa kijana cha miaka thenashar.

Baada haya Bwana wetu akamfufua mtu aliyekwisha kufa akazikwa tangu siku nne.

Alipokwenda Isa Yerusalemi, desturi yake kukaa katika nyumba ya mji Betania walipokaa mtu, jina lake Lazaro, na ndugu zake Maryamu na Martha, akawapenda wote. Lazaro akapatwa na ugonjwa, ndugu zake akapeleka kwa Isa, kumwambia, Bwana umpendaye hawezi.

Akisikia akangoja siku mbili, hatta baadaye akawaambia waanafunzi wake, Turudi Uyahudi. Waanafunzi wakaogopa, kwa sababu Wayahudi wamejaribu kumua. Akawaambia, Rafiki yetu Lazaro amelala, nnakwenda nimwamshe. Waanafunzi wakanena, Kulala ndio dalili ya kupona. Akawaambia kwa wazi, Lazaro amekufa, nami kwa ajili yenu nafurahi nisipokuwako huko mpate kuamini, illakini twende zetu kwake. Wakaenda, hatta walipofika amezikwa tangu siku 'nne.

Bassi Betania karibu na Yerusalemi, Wayahudi wengi wakaja kuhana na Maryamu na Martha, nduguze, wakakaa nyumbani wakilia. Akapewa habari Martha ya kwamba Isa anakuja. Akatoka akaenda kumwona, hatta akimkuta, akamwambia, Bwana, kama ungalikuwa-

po hapa, ndugu yangu hangalikufa, na hatta sasa utakalotaka Muungu atakupa. Isa akamwambia, Ndugu yako atafufuka. Akamwambia, Najua ya kwamba atafufuka siku ya kiyama. Isa akamwambia, Ndimi niliye ufufuo na uzima, aniaminiye mimi, hatta akiisha kufa, ataona uzima, naye aliye hayi aniaminiye hatakufa kabisa. Waamini haya? Akamwambia, Ndiyo, Bwana, naamini ya kuwa ndiwe Masiya, Mwana wa Muungu, aliyepasa kuja ulimwenguni.

Bwana wetu amkumbusha, ya kwamba kiyama na uzima kazi yake, wala pasipo yee hapana ufufuo wala uzima.

Martha akarudi kwa nduguye Maryamu, akamwambia kwa siri, Mwalimu amekuja, akuita wewe. Maryamu akaondoka akaenda kumwona. Wayahudi waliokuwako pamoja naye wakathani, aenda kaburini alie huko, wakamfuata. Wakamkuta Isa 'nje ya mji.

Maryamu akamwangukia miguu, akanena, Bwana, kama ungalikuwapo hapa ndugu yangu hangalikufa. Isa akiwaona wote wakilia, akataabika akasema, Mlipomlaza wapi? Wakamwambia, Bwana, njoo katazame. Isa akalia.

Wayahudi wakasema moyoni, Amempenda 'mno. Hakuweza kumzuia asife? Ametenda miujiza mingi. Wakaja kaburini, ndilo paango na jiwe limetiwa juu yake. Isa akanena, Ondoa jiwe. Martha akamwambia, Bwana, amekufa tangu siku 'nne. Aliona sasa ameoza haifai kumtazama. Isa akamwambia, Sikukuna ya kuwa ukiamini utaona utukufu wa Muungu? Wakaondoa jiwe.

Isa akamshukuru Muungu ya kwamba watu hawa wataona jambo kuu wapate kuamini. Akapiga kelele, Lazaro utoke! Aliyekufa akatoka mwenyi saanda na nguo za wafu. Isa akawaambia, Mfungueni aende zake. Hivi kwa neno lake akamfufua, akaonyesha ya kwamba ndiye aliye na nguvu juu ya kufa na kufufua. Wengi walioona wakamwamini.

Miujiza hii na mingi iliyoandikwa katika Anjili, na mingi isiyoandikwa, Bwana wetu aliitenda, watu wapate kujua ya kwamba ndiye, aliye na nguvu za Muungu.

SOMO XXV.

Mifano ya Bwana wetu.

Akifundisha Bwana wetu akaona watu wengi wasiofikiri, na wengi waliotaka kumuthi,

wakatafuta, katika maneno yake, sababu ya kumstaki. Kwa hiyo, akatumia sana mifano ao mithali, kasidi, watu wajifunze kufikiri wapate kuona maana yake, wala asiwape nafasi maadui wake.

Maana yake mfano ndiyo neno la kufanana. Watu wajua mambo ya dunia hii, mambo ya Muungu hawajui. Bwana wetu atufasiria mambo tusiyoyajua kwa mambo yaliyojulikana sana.

Kwanza amesema ya kwamba, Yee mwenyewe amefanana na mtu anayepanda mbegu. Dasturi ya inchi ile ilikuwa, kulima sana inchi kwa chombo kilichovutwa na ng'ombe, na tena kutupa mbegu kwa mkono, na kufunika kwa kuvuta kitu chingine juu ya inchi. Bassi mtu akitupa mbegu zake hazikuanguka zote katika mahali pema. Ngine zikaanguka juu ya njia, ngine katika mawe, na ngine katika magugu. Hivi Bwana wetu asema, neno lake lawafaa walio tayari moyoni walipokee, kama udongo uliolimwa, wangine wasiofikiri mioyo yao kama njia, mbegu haziingii, na ndege wakija huzila. Hivi shetani sikuzote tayari kuondoa neno kwao wasiofikiri. Watu wasio imara, wanaobadilibadili ni kama mahali pasipo udo-

ngo mwingi, wanasikia wanapendezwa sana, illakini marra moja wakisikia neno la pili, lile la kwanza limeshauliwa, kama mbegu katika mawe, huota, illakini mizizi yake haifiki chini, marra jua likichoma hukauka. Wako wangine wanaosema moyoni nikiisha shughuli zangu nitasikiliza; wangalipenda kuokoka illakini wataka kwanza kupata mali, ao kutenda shughuli ao kujizumgumza, na katika haya wasahau waliyoyasikia, nao wamekufa mbele hawajayafikiri. Ndio kama mbegu panapo miiba, miiba huota upesi, wala mbegu zikiota hazina nguvu za kuzaa.

Katika watu wanaosikia maneno, wanaojifanya Wamasihiya kuna watu wema, na watu wabaya, si woto walio wema, wangine wamegeuka tena kuwa wabaya, wangine hawakufikiri tangu mwanzo hatta mwisho. Hivi Bwana wetu anasema, Ufalme wa Muungu ni kama jarifa iliyotupwa baharini, imejaa samaki, ngine njema, ngine mbaya. Wavuvi hutupia mbali samaki mbaya, hivi siku ya mwisho malaika watafukuzia mbali wabaya katika kanisa la Muungu. Illakini sasa waana Adamu hawajui wapi walio wema, wala wapi walio wabaya. Hivi Bwana wetu anasema, Ufalme wa Muungu

ni kama mtu aliyepanda mbegu njema akaja adui usiku akapanda mbegu mbaya. Kama Muungu hututia mawazo mema, na shetani kwa siri hututia mabaya. Sasa hatuwezi kuondoa wabaya wote katika kanisa, kwa sababu hatujui sana mioyo ya watu. Illakini siku ya mwisho walio wa Muungu wataingia mbinguni walio wa Shetani watatupwa motoni.

Sisi waana Adamu hatuoni ginsi Muungu alivyotenda katika Kanisa akileta watu kwa wokovu. Bwana wetu anasema neno lake ni kama mbegu iliyopandwa, huota, illakini hatuoni ginsi inavyoota, ao kama chachu inayochacha mikate mingi, ao mbegu ndogo inayoota kuwa mti mkubwa. Twajua ndiyo, illakini ginsi ya kuwa hutujui. Wala hapana kitu kilicho cha thamani kuliko wokovu, ni kama shamba lilimofichwa fetha nyingi ao lulu iliyo nzuri mno, mtu wa akili angalikuza mali yake yote apate kuipata.

Illakini watu wengi wanapenda mambo ya dunia kuliko mambo ya mbinguni. Hivi Bwana wetu anasema, Ufalme wa Muungu ni kama Mfalme aliyefanya karamu kwa arusi ya mwanawe, akawaita wageni wengi. Illa hawa wameona killa mtu ana shughuli yake, hawezi kuja,

nao watumwa wa Mfalme wakisema nao, wakaona hasira wakawapiga, wakawafukuza. Hatta mfalme akisikia akapeleka ɲjiani na hatta mashamba, wakaleta watu wote waliowaona. Hivi Mayahudi wakikataa Anjili, wakiwapiga mitume, Muungu ameleta sisi watu wa mataifa tukae kitako mahali pao, na watu wote wanaopenda mno mambo ya duniani watafukuzwa katika mahali pao mbinguni.

Lakini watu wakitubu Muungu hanyimi kuwasamehe. Anasema ni kama mtu mwenyi watoto wawili aliyewapa killa mtu sehemu yake, mmoja akaenda zake akatawanya mali yake katika usherati na ulevi. Hatta akiona njaa, akafikiri, afathali ningalikuwa mtumishi katika nyumba ya baba wangu kuliko kukaa katika taabu hizi, akarudi, amenenyekea na amesikitika sana. Nayo Baba yake akimwona mbali akapiga mbio, akamkumbatia, akampa nguo na chakula, akafurahi sana. Sisi kama kondoo na mali ya Muungu, na mtu mwenyi kondoo, mmoja akipotea hutafuta sana, hatta akimwona humleta kwa furahi nyingi. Ao reale moja ikipotea mwenyewo hutafuta sana na kufagia na kumulika hatta akiiona hufurahi sana. Hivi malaika wa Muungu hufurahi, mtu aliyepotea katika thambi

akirudi kwa kutubu.

Wala watu walio wema wasijivune juu yao wasio wema. Kama mtu Mfarisayo aliyeshukuru Muungu ya kwamba hakukosa sana, wala siye kama mtu mwingine alioko. Yule mwingine hakuthubutu hatta kutazama juu illakini akaneua, Muungu anirehemu niliye na thambi. Naye Muungu amempenda yule aliyenenyekea kuliko yule wa kwanza mwenyi kiburi.

Wala watu wenyi mali wasijisifu kwa mali yao. Palikuwa na mtu mwenyi mashamba yaliyozaa sana hatta hana mahali pakuwekea mali zake, akaona, sasa nitastarehe miaka mingi nikila na kunywa. Illakini Muungu akamwambia, Hatta usiku huu roho yako itakuacha, itakufaa nini mali hizo? Palikuwa na mtu mwingine mwenyi mali, palikuwa na mwombaji aliyelazwa mlangoni pake. Hatta walipokufa, mwombaji akapewa mahali peponi, yule mwenyi mali akajiona motoni.

Sisi hapa tumepewa killa mtu riziki zake. Mmoja nyingi, mmoja chache. Ni kama mtu akisafiri aliyegawanya mali zake kwa watumwa wake killa mtu achume fayida kwa kadiri yake. Hatta akirudi waliotumia vema hupewa thawabu, wasiotumia hufukuzwa.

Wala hatujui wakati wa hukumu, ni kama vijana waliomngoja bwana arusi, wote wameleta taa, wangine wenyi akili wameleta tena mafuta, wasio na akili hawakuleta. Hatta usiku akija, walio na mafuta wakatengeneza taa zao wakaingia pamoja naye. Wasio na mafuta hawakuweza kuwasha taa zao, wala hawakupata kuingia kabisa. Hivyo wasio tayari siku ile hawapati kukaa na Bwana wetu.

Hatta siku ya mwisho, watu wema na wabaya watagawanyika na malaika, kama kondoo na mbuzi na mchunga, nao walio wema wataitwa mbinguni, nao wasio wema watafukuzwa motoni.

SOMO XXVI.

Utukufu wa Bwana wetu.

Bwana wetu alikaa hapa duniani kama mtu maskini, illakini marra kwa marra utukufu wake wa Muungu ulionekana. Kama alipozaliwa malaika wakajâ wakaimba, nuru ya mbinguni ikaonekana. Tena nyota ikaangaza, ikawaleta wamajusi na tunu zao. Tena akibatizwa, sauti ikasikiwa katika mbinguni kumwita Mwana wa Muungu. Tena akisema na wageni Wayonani, akanena, Baba, utukuze jina lako. Sauti

ya mbinguni ikamjibu, Nimekwisha kulituku-za, nami nitatukuza tena. Sauti hii kuu, hat-ta watu wasiotambua maneno yake wakanena kuna ngurumo.

Illakini utukufu wake ulipoonekana sana ndipo, alipotwaa Petro, na Yakobo, na Yohana, akapanda mlimani kuomba, uso wake ukageu-ka, nguo zake zikang'aa kama isivyo yamkini hapa duniani. Wakatokea watu wawili waki-sema naye. Watu hawa ndio Musa na Eliya. Musa, aliyetoa torati na sheria kwa Waisraeli, na Eliya, aliye mkuu wa manabii. Mitume waliopo huko pamoja naye wakarukwa na akili, wakiona utukufu wake na watu walioseina naye. Hatta Petro akamwambia, Mwalimu, hapa pe-ma, tujenge hapa masikani tatu, mcja wako, mo-ja wa Musa, moja wa Eliya. Hatta akiwa katika kunena wingu jeupe likawatia kivuli, wakasikia sauti ikinena, Huyu Mwanangu nimpendaye, msikieni. Na wingu likipita hawakuona mtu tena, illa Isa peke yake. Mambo waliyoyane-na Musa na Eliya ndiyo mambo ya kufa kwa-ke, naye akawaagiza waanafunzi wake wasi-mwambie mtu illa atakapokwisha kufa. Aka-nena, Mambo haya yatulie masikioni mwenu, kwani Mwana Adamu atatolewa mikononi mwa

watu, nao wetamua.

SOMO XXVII.

Siku za mwisho za duniani za Bwana wetu.

Wakati umekaribia ilipompasa Bwana wetu afe. Miaka mitatu imepita tangu alipobatizwa na Yohana. Killa mwaka kwa siku kuu huenda Yerusalemi, kama ilivyoamuru Torati. Hatta mwaka huu akaenda vivyo kwa siku kuu ya Pasaka, kwani Muungu ameamuru siku ileile walipookoka Waisraeli katika utumwa wa Misri, sisi waana Adamu tuokoke katika utumwa wa thambi na kufa.

Isa akafika karibu na Yerusalemi siku ya juma akaenda kukaa wakati wa karamu nyumbani mwa Lazaro, aliyemfufua katika wafu. Watu wengi wakaja kumtazama Isa na kumwona Lazaro. Hatta walipoleta chakula, Lazaro akakaa mezani pamoja naye, na Martha akawasimamia watumishi. Illa Maryamu, aliyezidi sikuzote kumpenda Isa, akaleta kibweta cha marhamu mzuri sana, ya thamani nyingi, akamtia miguu, hatta nyumba yote ikajaa manukato yake.

Waanafunzi wakaona ajabu, wakathani Bwana wao hangalipendezwa, na mmoja wao, Yuda

Iskariota, mtu wa choyo, akanena, Mbona marhamu haikuzwa? na maskini wangalipewa thamani yake, ndiyo dinari mia tatu. Illa Isa akajibu, Mwacheni, kwa kuzikwa kwangu ameitenda, na killa itakapohubiriwa Anjili tendo lake hili litanenwa kwa heshima yake. Mnao sikuzote maskini, mimi sikuzote hamnami.

Bwana wetu amewaambia waanafunzi marra nyingi ya kwamba atauawa na baadaye atafufuka, illakini hatta mwisho hawakufahamu, hivi sasa amwakumbusha, akikubali gharama hii ya Maryamu, si kwa anasa, wala kwa kiburi, illa kwa kujiweka tayari aingie kaburini. Kwani dasturi ya siku zile kuwatia wafu manukato mengi wakati wa kuzikwa.

Watu waliomfuata Isa wakamsifu sana kwa tendo kuu alilomtendea Lazaro, na watu wengi wasiomfuata wakamthania, ndiye nabii. Illakini watu waliomchukia wakazidi kumchukia, wakafanya shauri wamue na Lazaro, kwa sababu akiwa hayi amekuwa shahidi mkuu wa nguvu zake Isa.

Siku ya juma a pili.

Betania ni karibu sana na Yerusalemi, lakini mji hauonekani katika Betania, kwa sababu

ya mlima wa Zeituni ulio kati. Njia ikitoka Betania yapanda katika mlima Zeituni, ikizunguka katika mlima hatta kama nussu ya njia, marra moja mji mkuu umeonekana na hekalu ya Muungu, uko umelekea mlima wa Zeituni, na boonde kubwa katikati. Watu waliokwenda kwa siku kuu ya Pasaka wakiona hekalu, marra wakaanza kuimba zaburi na kumsifu Muungu.

Hatta Isa akitaka kwenda Yerusalemi watu wengi wakafuatana naye. Akapeleka waanafunzi wawili kumletea punda, katika mji mgine, akawaambia mahali watakapomwona, na ya kwamba wenyewe wakisikia ya kuwa amtaka watampeleka. Wakaenda wakamleta mwana punda, wakatandika nguo juu yake, wakampandisha Isa, wakaenda zao mjini.

Hatta wakienda, watu wakaanza kuimba kwa heshima yake maneno ya zaburi, kunena, Amebarikiwa ajaye kwa jina la Yahuwa. Wakaweka nguo zao katika njia, apite juu yao kama juu ya zulia, na wangine wakakata matawi ya miti wakayaandika njiani, wakazidi kumwimbia. Naye akiona mji katika uzuri wake, hakufikiri uzuri wa mawe yake, illa ugumu wa moyo yao waliokaa humo. Akiutazama akalia, akanena,

Laiti ungalijua hatta leo mambo ya amani yako, hatta sasa yamestirika kwako, maadui yako watakuangusha pia, kwa sababu hujui wakati wa kujiliwa kwako. Hatta sasa, na hatta waliomwimbia hawakujua ya kuwa ndiye Mwokozi wao.

Akifika mjini, watu wote wakashangaa wakanena, Nani huyu? Wafuasi wakawajibu, Ndiye Isa nabii wa Nazareti.

Hatta hekaluni watu wakamfuata wakamwimbia, nao maadui wake walipomtaka wanyamaze, akawaambia, Kama hawa wangenyamaza hatta miti na mawe yangalipiga sauti.

JUMA A TATU HATTA JUMA A TANU.

Bwana wetu akaenda killa assubui kuabudu na kufundisha katika hekalu, na killa jioni hurudi Betania. Akienda mjini akaona njaa, akaenda mtini uliojaa majani atafute matunda. Lakini matunda hapana. Akamwambia, Usizae tena matunda milele. Ndio mfano wa mji wa Yerusalemi, uliokuwa mzuri ukajaa watu waliosema ya kwamba wamtazamia Masiya, illakini Masiya akija, wakamua. Majani yafanana na maneno mema, matunda yafanana na matendo. Bwana wetu ametoa zamani mfano wa mtini

usiozaa, kwa maana ya mtu aliyejifanya mwema, akiwa ndani hafai.

Siku ya pili wakipita njia ileile, wakaona ya kuwa mtini umenyauka pia.

Akaingia hekaluni akaona humo watu waliovunja fetha na watu waliokuza ng'ombe, na kondoo, na hua, kwa wageni waliotaka kutoa thabihu, akawafukuza wote akiwaambia, Nyumba hii nyumba ya kuomba, si nyumba ya kupata fayida kwa udanganifu, kama dasturi ya watu wanaofanya biashara na wageni.

Wakohani wakuu wakamwona amefukuza watu katika hekalu, na watu wote humfuata, wakaona hasidi. Wakamkuta hekaluni, wakamuliza, Kwa uwezo gani wafanya haya, nani aliyekupa nguvu hii? Akajua ya kwamba hawakuuliza kwa nia ya kujifunza illa kwa moyo mbaya. Akawaambia, Nijibu mimi swali moja, tena nitawaambia, Ubatizo wa Yohana, jambo la mbinguni, ao la mwana Adamu? Hawakuthubutu kumjibu kama Yohana nabii, kwa sababu Yohana ndiye aliyesema, Huyu ni Masiya. Akiwa Yohana nabii, Isa yakini mfalme wao. Wala hawakuthubutu kusema, Yohana siye nabii, kwa sababu ya watu, waliomkubali wote. Wakanena, Hatujui. Hila yao ikapotea.

Isa akatoa mifano juu yao. Kwanza wa mtu aliye na waana wawili. Akamwambia wa kwanza, Enenda nitendee kazi, akakataa, illakini halafu akatubu akaenda. Akamwambia wa pili, akanena, Nnakwenda, Bwana, illakini hakwenda. Huyu kama watu wakuu wa Wayahudi waliotoa maneno mema sana wasitende kabisa. Yule wa kwanza kama watu wabaya waliosikia maneno ya Yohana wakatubu, wakaokoka.

Akawaambia tena mfano wa mtu aliyeteugeneza shamba lake, akalipangisha kwa watu wakulima, nao alipotaka kodi, wakawapiga watumwa wake wakawafukuza, hatta mwisho akampeleka mwanawe, wakamua. Hivi Wayahudi wakawafukuza nabii za Muungu, hatta akija Mwana wakamua.

Wakaja tena wamfanyie hila wapate kumstaki kwa maneno yake. Warumi wamewashinda Wayahudi, mfalme wa Rumi, aliyeitwa Kaisari, akatwaa kodi na ushuru kwao. Illakini waliojifanya watakatifu wakasema ya kwamba Muungu ndiye mfalme wa Israeli, wala si halali kumpa kodi na ushuru Kaisari, aliye mgeni na kafiri. Wakamwuliza Bwana wetu kama halali kutoa kodi kwa Kaisari ama sivyo. Waliona akisema, Ndivyo, tutamstaki kwa kumwasi

Muungu. Akisema, Sivyo, tutamstaki kwa Warumi.

Bwana wetu akajua mioyo yao akanena, Kwa nini mwanijaribu? Niletee fetha ya kodi. Wakamletea dinari iliyopigwa na Warumi. Akawaambia, Mpe Kaisari yaliyo yake, na Muungu yaliyo yake. Kumpa Kaisari fetha aliyoifanya mwenyewe ni halali, lakini moyo na roho ni mali yake Muungu.

Wangine wakamjaribu kwa maswali, akawajibu wote. Hatta halafu akawauliza neno moja. Masiya ni Mwana wa nani? Wakanena, Wa Daud. Akauliza, Kwa nini Daud amemwita bwana wake, akinena katika Zaburi cx, Yahuwa akamwambia Bwana wangu, uketi mkono wangu wa kuume? Wala hawakuweza kumjibu. Hivi akawaambia ya kwamba ndiye Muungu. Kwani twajua ndiye mwana wa Daud, akiwa mtoto wa mamaye Maryamu, naye Bwana wa Daud, akiwa Neno la Muungu.

Akitoka mjini waanafunzi wakamwonyesha majengo ya hekalu yaliyo maajabu ya ulimwengu wote, kwa kuwa makubwa na mazuri. Akawaambia ya kwamba wakati karibu, yatakapoangushwa pia. Waanafunzi wakaulizia dalili za wakati ule na za mwisho wa ulimwengu. A-

kawaambia, ya kwamba yatakuwa vita, na njaa, na taabu katika ulimwengu, nao waliomfuata watachukiwa na watu wote. Akawaonya wakiona maadui wamezunguka Yerusalemi, wakimbie wapate kujiokoa. Akawaambia ya kwamba siku ya mwisho ndiyo siri ya Muungu, isiyojulikana na waana Adamu, illa kazi yao, kukesha na kuwa tayari.

Mambo haya yakiwa, maadui yake wakafanya shauri wamkamate kwa siri, kwani mchana na panapo watu hawakuthubutu kumtia mikono. Wakaona mmoja wa wathenashara aliye na choyo sana, ndiye Yuda Iskariota, wakamwambia, ya kwamba watampa fetha thelathini akiwaonyesha mahali alipo Isa peke yake, wapate kumkamata usiku na kwa siri; akapatana nao, akangoja nafasi amtoe.

Siku za Alhamisi na Juma.

Siku ya Alhamisi ndiyo mwanzo wa Pasaka, waanafunzi wake wakamwuliza, Tufanye wapi Pasaka? Akawaambia waende mjini, huko watamwona mtu anachukua mtungi, wamfuate hatta nyumba atakamoingia, huko wamwulize mwenyi nyumba, Wapi mahali pa wageni?

Wakaenda, wakauliza, wakapewa orofa kubwa iliyowekwa tayari. Ndiyo amri ya Pasaka, killa nyumba watoe mwana kondoo aliye mzuri, wamchinje hekaluni, waoke nyama yake kwa moto, wale usiku pamoja na mboga uchungu na mikate isiyochachwa, wala si halali kula, isipokuwa katika Yerusalemi. Kwa hiyo wakaenda mjini usiku ule, wala hawakurudi jioni Betania.

Wakaweka tayari, wakaja jioni wale Pasaka pamoja. Walipokuwa wamekuja, Bwana wetu akatwaa maji na kitambaa, akawaosha miguu waanafunzi wake. Kwanza wakaona haya wakakataa, illakini akiwaambia asipowaosha hawana sehemu naye, wakakubali. Akawaambia, ya kwamba yee mkuu wao amewaosha miguu, makusudi wapendao kuwa wakuu wajifunze kunenyekea kwa namna yake.

Hatta walipokuwa wamekula akatwaa mkate akauvunja akawapa, akiwaambia, Huu ni mwili wangu, uliotolewa kwa ajili yenu. Akawapa tena kikombe chenyi mvinyo, akiwaambia, Hiki ni damu yangu iliyotolewa kwa ajili yenu, na kwa ajili ya wengi, iliyomwagika kwa kuondolewa thambi. Akawaamuru wafanye kama alivyofanya yeye, kwa kumkumbuka. Hii

ndiyo siri ya Chakula cha Bwana wetu, tunayofanya killa siku makanisani mwetu. Tumeambiwa na mtume Paolo, ya kwamba killa tulapo mkate huu tumeshariki mwili wa Bwana wetu, na killa tunywapo mvinyo tumeshariki damu yake, na maana ya siri hii ni kuonyesha kufa kwa Bwana wetu hatta atakapokuja tena, siku ya mwisho, na kufa kwake ni wokovu wetu na upatanisho wetu na Muungu.

Isa akawaambia waanafunzi wake, maneno mengi na mazuri, yaliyoandikwa katika Anjili ya Yohana, akawaombea sana, kwani akajua ya kwamba sasa atawaacha, nao watatiwa hofu nyingi na huzuni.

Hatta katika kula amewaambia ya kwamba mmoja wao atamtoa kwa adui zake. Wakaona wote sivyo, wakauliza killa mtu, Ni mimi? Akaonyesha Yuda Iskariota, akamwambia afanyalo afanye upesi. Hatta hivi hawakujua maana, illakini walithani shughuli yake Yuda kugawanya kwa masikini, ao kununua vifaa vya siku kuu.

Wakiisha kula, wakaimba zaburi, wakatoka mjini, wakashika njia ya Betania, hatta wakafika mahali palipoitwa Gethsemane, maana yake, kinu cha mafuta, palipo bustani walipozoea

kwenda. Wakaenda wakaingia katika bustani. Naye Yuda amejua ya kwamba walikuwa wakienda Gethsemane, akaenda akatwaa rushwa yake, akawaambia Wakohani wakuu, ya kwamba wakileta asikari watamwona huko Isa peke yake, pasipo watu wengi.

Isa akiona moyoni Yuda anakwenda, na mambo yote yatakayompata, akahuzunika sana, akawaambia waanafunzi waombe sana.

Akatwaa wateule wake watatu, Petro, na Yakobo, na Yohanna, akajitenga kidogo. Akaenda akaomba kwa bidii, hatta hari yake kama matone ya damu yaliyotoka kwake. Na maneno ya haja yake, Baba, ukipenda, uniondolee kikombe hiki, illakini ulipendalo wewe silo nilipendalo mimi. Akaja malaika akamtia nguvu. Akarudi kwa waanafunzi wake marra tatu, akawaona katika usingizi, kwani macho yao mazito. Akawaamsha, akawaambia, Anitoaye yuko karibu.

Akaja mtoa, na asikari na watu, akamsalimia Bwana wake, akambusu. Isa akamwambia, Yuda, wamtoa Mwana Adamu kwa kumbusu? Petro akafuta upanga akampiga mtumishi wa mkohani mkuu akamkata sikio. Isa akamgusa akamponya. Waanafunzi wote wakakimbia.

Askari wakamkamata Isa, wakamleta kwa mkohani mkuu.

Kwa sheria ya Musa mkohani mkuu ndiye mwana wa Haruni aliye mkubwa. Illakini siku zile Warumi wameondoa mkohani, wakaweka mgine mahali pake, killa walipopenda. Hivi mkohani mkuu wa mwaka huu, Kayafa, illakini aliye mkuu wa jamaa yake, Anna mkwewe Kayafa. Wakamleta Isa kwanza kwa Anna, na halafu kwa Kayafa, wakamtendea vibaya vingi.

Bwana wetu amemwambia Petro ya kwamba usiku ule mbele ya kuwika jogoo atamkataa marra tatu. Petro akanena, Sivyo, hatta nijapo kufa pamoja nawe. Bassi Petro na Yohanna wakamfuata mbali, waone yatakuwaje, wakaingia katika nyumba ya mkohani mkuu, huko watu walioko wakamwambia Petro, Ndiwe mwanafunzi wake. Akanena, Simjui. Hatta marra tatu. Naye akisikia jogoo anawika akakumbuka maneno ya Isa, akatubu sana, akalia mchozi machungu.

Assubui mapema, wakawaita wazee wote, wakafanya baraza wamhukumu Isa. Wakawaita mashahidi, watu wengi wakaja, wakanena maneno mengi ya uwongo, illakini hawaku-

weza kupata ushahidi utoshao kumhukumia. Wala yeye hakujibu neno. Hatta wakiona mashaka mengi, mkohani mkuu akamwapiza, Utuambie, ndiwe Masiya, ama sivyo. Akawaambia, Ndivyo, nanyi mtamwona halafu Mwana Adamu akija katika mawingu ya mbinguni. Wakanena, Bassi tumesikia, amejifanya Muungu. Mkohani mkuu akawauliza, Mwaonaje? Wakanena, Tumemhukumia kufa. Watu waliomzunguka wakampiga, wakamshutumu, wakamtemea mate.

Illakini Warumi ndio waliotawala Uyahudi, wala Wayahudi hawana ruksa kumua mtu, isipokuwa kwa amri ya liwali. Kwa sababu hiyo wakamleta kwa liwali, jina lake Pontio Pilato, wakamwambia, Huyu mtu mbaya, astahili kufa. Pilato akauliza, Kwa nini? Wakanena, Anawapotoa watu, awazuia wasimlipe kodi Kaisari. Maneno haya maneno ya uwongo, naye Pilato akamulizia tena, wala hakuona hatiya kwake. Isa akanyamaza kimya.

Pilato akauliza, Inchi yake ipi? Wakamwambia, Galilaya. Bassi siku hizi Herode ndiye aliye mfalme wa Galilaya. Pilato akampeleka kwake. Herode akafurahiwa, akataka kumwona akitenda mwujiza, akamwuliza mambo me-

ngi, wala Isa hakumjibu neno. Herode na askari zake wakamfanyia thihaki wakamleta tena kwa Pilato.

Pilato alitaka sana kumokoa, akawaambia watu, ya kwamba atamwacha, kwa dasturi ya siku kuu ile, kuwaachia mtu mmoja aliyefungwa. Wakapiga kelele, Si huyu, illa Barabba. Na Barabba mtu mnyang'anyi na muuaji. Pilato akajaribu tena kumwokoa, illakini wakafanya uthia mwingi hatta akaogopa kumwacha, akatwaa maji akanawa mikono mbele yao, akanena, Damu yake juu yenu wala si juu ya mimi. Wakajibu, Juu yetu na wazao wetu. Pilato akaamuru asulibiwe. Imekuwa kama saa ya tatu walipomtwaa asikari Warumi wakampiga kwa dasturi yao kuwapiga watu waliohukumiwa kufa, halafu wakamleta 'nje ya mji pamoja na watu wawili walio wanyang'anyi, wakawasulibisha wote mahali palipoitwa Golgotha. Wakamtia Isa katikati, wakaandika juu ya msalaba wake mstaka wake, "Isa wa Nazareti, Mfalme wa Wayahudi."

Isa akaona walipomkaza msalabani, Baba uwasamehe, hawajui watendavyo.

Wakaja mama wake Maryamu, na mwanafunzi aliyempenda, Yohanna, wakasimama kari-

bu na msalaba. Aka'mweka mamaye mkononi mwa Yohanna, amtunze kama mama wake yeye. Naye Yohanna tangu siku ile akamtwaa nyumbani mwake.

Watu na wakuu wa Wayahudi wakamthihaki, wakamwambia afathali ajiponye, ashuke msalabani, na mambo mangine mengi, hatta wanyang'anyi wakamwambia, Ujiponye mwenyewe na sisi. Mmoja wao akamshutumu tena, illa mwenzake akamkaripia, akanena, Sisi tumeteswa kwa haki, huyu hana hatiya. Akamwambia Isa, Bwana unikumbuke ukiingia katika ufalme wako. Isa akamjibu, Leo utakuwa peponi pamoja nami.

Hatta kama saa ya sita likawa giza juu ya inchi yote hatta saa ya tissa. Watu wakashangaa wakiliona giza.

Kama saa ya tissa, Isa akalia, Eli, Eli, lama sabakhthani, ndiyo maneno ya kwanza ya zaburi ya asharini na mbili. Akanena tena, Naona kiu, mtu mmoja akampa kunywa siki. Akanena tena, Imekwisha, akapuzia roho.

Hatta asikari Warumi wakiona wakanena, Ndiye mtu wa haki.

Wakaja asikari wakawavunja miguu wanyang'anyi, wapate kufa upesi, illakini wakimwo-

na Bwana Isa amekwisha kufa, hawakumvunja miguu, illa mmoja akamchoma mbavuni kwa mkuke.

Hatta katika wakuu wa Wayahudi walikuwa waliomwamini Isa, illa wamejificha kwa hofu. Mmoja wao, Yusuf wa Arimathayo, akaenda kwa Pilato, akataka ruksa atwae mwili wake Isa katika msalaba, amzike. Akapewa na Pilato, akaenda, akaushusha, akauweka katika kaburi jipya alilojifanyia karibu na mahali Golgotha. Akaja tena Nikodemo, akaleta manukato. Wakatia jiwe lililo kubwa mlangoni mwa kaburi, wakaenda zao, wakastarehe siku ya Sabato.

Siku ya Juma a pili.

Bwana wetu akiisha kufa waanafunzi wake wakakata tamaa, hawakukumbuka maneno yake, alipowaambia marra nyingi ya kwamba atakufa, na baada ya siku tatu atafufuka. Lakini adui zake hawakusahau, wakaenda kwa Pilato, wakataka askari, wapate kulilinda kaburi, mtu asipate kuondoa mwili wake.

Siku ya Juma jioni wamemtia kaburini kwa haraka, waanaake walio jamaa zake wakaweka tayari manukato na vifaa, wapate kuutunza mwili wake. Hatta siku ya juma a pili alfajiri

wakaenda kaburini watende kazi yao. Walikumbuka jiwe ginsi lilivyo kubwa, wakathani labuda hatutoshi kuliondoa. Illakini wakifika wakaliona kaburi wazi, wala hapana mwili ndani.

Kwani marra, siku ya tatu ikianza, palikuwa tetemeko kuu, asikari wakatiwa hofu nyingi, wakaona malaika akishuka na kuondoa jiwe, naye Isa amekwenda zake. Hivi asikari waliotiwa wamzuie asiondoke kaburini wamekuwa mashahidi wa ufufuo wake.

Waanaake walikuja kwanza kaburini ndio Maryamu Magdalene, na Maryamu wa Yakobo, na Salome, wakitazama wakaona malaika, aliyewaambia, Msiogope, mwamtafuta Isa aliyesulibiwa, hako, amefufuka, kama alivyosema. Wakaenda mbio wakiogopa sana. Illa Maryamu Magdalene akakaa karibu na kaburi akilia, hatta mtu akamwambia, Walilia nini? Yee akithani ndiye aitunzaye bustani, akamwambia, Kama umemwondoa hapa, niambie umemweka wapi? Akamwambia, Maryamu! Marra akamtazama, akamjua kama ndiye Isa. Waanaake wangine wakamwona njiani. Petro na Yohanna wakaja upesi wakaona kaburi li wazi, wakaanza kukumbuka maneno yake.

Baadaye akaonekana na Petro. Na jioni akafuatana na wawili wao waliokwenda Emmao. Kwanza hawakumjua, hatta wakimtambua wakarudi upesi Yerusalemi, wakaona waanafunzi wamekusanyika, wakawaambia. Hatta wakinena, Isa mwenyewe akaja akawaonyesha miguu na mikono yake, palipopenya mismari msalabani.

Illakini mmoja wao, Tomaso, hakuwako, akaona shaka, wala hakusadiki sana. Akanena, Sina buddi kutia kidole katika mahali pa mismari na mkono mbavuni ulipoingia mkuke wa askari, ndipo nitakaposadiki. Baada ya siku saba walikuwako pamoja na Tomaso, Isa akawajia, akamwambia Tomaso, Nyoshe kidole, kanitie mkononi, nyoshe mkono, kanitie mbavuni, wala usikatae kuamini. Tomaso akimwona mwenyewe, akamwangukia akanena, Bwana wangu, na Mungu wangu.

SOMO XXVIII.

Kupaa Bwana wetu mbinguni.

Siku arobaini baada ya kufufuka Bwana wetu amekuwapo juu ya inchi, akiwatokea waanafunzi wake. Illa si kama kwanza. Kwanza alikuwa kama sisi wote, akichoka, akiona njaa,

na akilala, baada ya kufufuka hakuna mtu aliyemwona amechoka, ao amelala. Watu hawakumwona kuingia ama kutoka. Marra yuko, marra hako, hatta milango ikifungwa.

Waanafunzi walirudi Galilaya baada ya Pasaka, huko wakamwona katika mlima aliotangulia kunena. Siku moja alionekana na watu hatta hamsi mia pamoja. Tena akaonekana na mtu mmoja tu.

Siku moja Siman Petro, na Yohanna na waanafunzi wangineo wakaenda kuvua samaki. Wakatenda kazi usiku kucha wasipate kitu. Hatta assubui wakamwona mtu pwani aliyeuliza kama wamepata chakula. Wakamwambia, Hakuna. Akawaambia, Tupeni jaarifa upande wa kuume, mtapata. Wakatupa wakapata samaki wengi mno. Yohanna akamwambia Petro, Ndiye Bwana, Petro akajitupa majini afike upesi kwa Bwana wake. Wakaja wakaona chakula tayari, wakakaa kitako kula na kuzumgumza. Hatta wakiisha, Isa akamwambia Petro, Siman wa Yunus, wanipenda mimi? Akajibu, Yakini, Bwana, wajua nakupenda. Akamwambia, Walishe waana kondoo wangu. Akamwambia tena, Siman wa Yunus wanipenda mimi? Akajibu, Yakini, Bwana, wajua

nakupenda. Akamwambia, Uchunge kondoo zangu. Akamwambia marra ya tatu, Siman wa Yunus, wanipenda mimi? Petro akatiwa huzuni akimwambia marra tatu maneno yaleyale, akamwambia, Bwana, wajua yote, wajua nakupenda. Akamwambia, Ulishe kondoo zangu. Akamwambia Petro tena mambo yatakayompata halafu.

Akiwa pamoja na waanafunzi wake Bwana wetu akawaambia, Kama Baba wangu alivyonituma mimi, hivi nawatuma ninyi. Akawaambia tena, Enendeni katika ulimwengu wote, 'mwafundishe mataifa yote, nikiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu. Aaminiye akibatizwa ataokoka, asiyeamini atapotea. Akawaambia tena, Mimi pamoja nanyi hatta mwisho wa ulimwengu.

Siku arobaini zikiisha walikuwa wote pamoja katika Yerusalemi. Akawaagiza wakae katika Yerusalemi hatta watakapopewa iliyoahidika, ndiyo Roho Mtakatifu.

Wakatoka mjini kwenda mlima wa Zeituni. Wakamwuliza, kama atarudisha siku zile ufalme kwa Israeli. Akawaambia, wasifikiri mno wakati aliouweza Muungu tu, illakini wakipewa nguvu kwa Roho Mtakatifu watamshuhudia

katika Yerusalemi, na Samaria, na ulimwengu wote.

Hatta wakitazama, akachukuliwa juu, wingu likampokea wasimwone tena. Hatta wakisimama wakitazama mbinguni, wako watu wawili wamesimama nao, wenyi mavazi meupe, wakawaambia, Enyi watu wa Galilaya, kwa nini wasimama wakiangalia juu mbinguni? Huyu Isa aliyechukuliwa juu katika kwenu atarudi tena, kwa ginsi hiyo mlivyomwona kwenda mbinguni.

Mwisho.